# Nipashe

Ijumaa Septemba 18, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580342

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US




## Afungwa jela miaka 30 kwa kumbaka mtoto wa kumzaa

UKURASA 4




UKURASA 11

# KAA CHONJO

• **DPP** akunjua makucha kufyeka uhalifu, ukikamatwa na wahamiaji haramu nyumba kutaifishwa, ukiwasafirisha unanyang'anywa gari, watoroshaji madini, wabakaji kukiona, aonya wanaosaka wachumba mtandaoni... *Endelea ukurasa 2*



Mgombea Urais kupitia chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), Queen Cuthbert Sendiga, akisalimiana na wananchi wa Pemba kabla ya kuhutubia mkutano wake wa kampeni juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mgombea Urais kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mgahywa, akizungumza kwenye mkutano wa kampeni, Tegeta jijini Dar es Salaam jana na kuomba wananchi wamchague ili aimarishe kilimo na viwanda nchini. **PICHA: SABATO KASIKA**

## IPP yang'ara kinyang'anyiro tuzo uandishi EJAT 2019

UKURASA 5

## Kasi ya kusaka kura urais yapamba moto

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

VOTE

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Wafanyakazi wa Geita Gold Mine Ltd, wakizungumza na wageni wanaotembelea banda la kampuni hiyo lililopo katika maonyesho ya teknolojia ya madini mjini Geita jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kaa chonjo makucha ya DPP

**Na Mwandishi Wetu**

KAA chonjo! Ndivyo unavyoweza kusema kuwapa tahadhari watu wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu walivyo katika hatari ya kufungwa jela na mali zao kutaifishwa.

Katika kikao chake na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, alisema mikakati yao imekuwa na mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na kudhibiti ukatili dhidi ya watu wenye ualbino nchini.

"Kwa sasa tukikukamata unasafirisha wahamiaji haramu, tunachukua gari, tukiwakuta nyumbani kwako, maana yake ni kwamba umeshindwa kuitumia vizuri nyumba hiyo, itataifishwa ili kutoa fundisho kwa jamii," alisema.

Mganga alibainisha kuwa wamefanikiwa kwa kiwango kikubwa kudhibiti wizi wa mtandao, lakini akatahadharisha kuwa wasichana wanaotumia mitandao ya kijamii kutafuta wachumba kwamba kuna hatari ya kuingia kwenye hatari ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia na kutapeliwa na makundi yanayotumia mwanya huo.

Alisema wapo pia wazazi wanaoshirikiana na wanaume aliowaita wabakaji, kuwaoza binti zao au kuharibu ushahidi wa watoto wao kubaka, akionya kuwa kwa sasa kinachofanyika ni "kuweka ndani" wazazi wa aina hiyo.

Mkurugenzi huyo pia aliwataka wananchi wenye kero mbalimbali zinazoigusa ofisi yake, ikiwamo kuchelewa kwa upelelezi na watuhumiwa kuwekwa mahabusu kwenye selo za polisi, kufika kwenye ofisi zao zilizoko katika maeneo mbalimbali nchini kutoa malalamiko yao, akiahidi yatashughulikiwa haraka.

Mkurugenzi wa Divisheni ya Utakatishaji wa Mali, Makosa Yanayovuka Mipaka na Uhalifu Mahsusi, Paul Kadushi, alisema wamepata mafanikio makubwa katika kudhibiti ujangili nchini, akibainisha kuwa nchi iliamua kuchukua hatua za haraka baada ya kubaini kuwa hadi mwishoni mwa mwaka 2014, asilimia 60 ya tembo nchini walikuwa wameuawa na majangili.

"Katika kipindi cha miaka mitano, tumewezesha nchi kupata amri ya kutaifisha mali zilizotokana na utoroshaji wa madini na ujangili, tunajisikia furaha kwa hili. Magari 143, pikipiki 163, nyumba 23 na viwanja 10 kikiwamo cha ekari tano eneo la Buhongwa Mwanza, zimetaifishwa.

"Kwenye madini, tumetaifisha tani 84.07 zenye thamani ya Sh. bilioni 45.82. Kati yake, madini ya vito ni tani 83.596 yenye thamani ya Sh. bilioni sita na Kg 425 za dhahabu zenye thamani ya Sh. bilioni 38.9. Pia tumetaifisha magogo 18,409 yenye thamani ya Sh. bilioni 1.15," alibainisha.

Mkurugenzi wa Divisheni ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi, Hashim Ngole, alisema mafanikio mengine ya ofisi hiyo ni kuharakisha upelelezi wa kesi, akitolea mfano kesi ya mwalimu kumuua mwanafunzi kwa kipigo mkoani Kagera mwaka jana, ambayo iliendeshwa kwa muda mfupi.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wanapunguza msongamano wa mahabusu kwenye magereza mbalimbali nchini, waliwezesha kufanyika kwa marekebisho ya sheria ili kuweka kifungu kinachoruhusu watuhumiwa kukutana na DPP na kuomba kukiri makosa yao.

Katika mkutano huo, DDP Mganga aliulizwa sababu za watendaji wake kufanya upekuzi nyumbani kwa watuhumiwa wa makosa ya uchochezi, akijibu kuwa wanafanya hivyo ili kujiridhisha kama mtuhumiwa ana vitu nyumbani ambavyo huenda vinasababisha atoe kauli za aina hiyo.

"Huenda mtu anavuta bangi ndiyo maana anatoa kauli za kichochezi, kwa hiyo watapekua nyumbani kwake ili kujiridhisha kama anatumia dawa hizo. Kikubwa, ukitaka kuishi kwa amani tii sheria tu, basi!" Mganga alionya.


Total Fiscal Solutions

**TANGAZO KWA UMMA**

Tulishatangaza kuwa **Ipyana Mwandete** siyo Mfanyakazi wa **TOTAL FISCAL SOLUTIONS** tangu tarehe **6/8/2018.** Tunaomba walipa kodi waliopewa risiti zisizo halali **(EFD)** wafike ofisi ya **TRA Mbeya** ndani ya siku saba (7) kuanzia tarehe ya tangazo hili pamoja na nyaraka zinazohusiana na mauziano hayo.

**Kwa taarifa Zaidi naomba piga namba 0755 225970 au barua pepe helpdesk@totalsolutions.co.tz**

215905602


# JPM atamba kufanya makubwa Kigoma

**Na Gwamaka Alipipi,** KASULU

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, ametamba kufanya mambo makubwa ya kimaendeleo katika mkoa wa Kigoma, mojawapo ni kujenga miundombinu ya kisasa itakayounganisha mkoa huo na nchi za Afrika.

Akiwa katika uwanja wa Kiganamo wilayani Kasulu jana, Dk. Magufuli alisema mkoa wa Kigoma umetengewa Sh. bilioni 402 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kisasa, ikiwamo ujenzi wa barabara kutoka Kibondo-Kasulu-Namanyovu (kilometa 260).

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo serikali inamkakati wa kujenga barabara itakayounganisha Sudani Kusini-Uganda-Mtukula-Biharamulo-Kakonko-Kasulu- Kigoma-Uvinza-Mpanda-Sumbawanga-Tunduma-Zambia-Zimbabwe-Afrika Kusini, kwamba barabara hiyo itaanzia Kasulu.

"Nazifahamu kero za wananchi wa Kasulu, nafahamu shida zenu, nilipoingia madarakani mwaka 2015 changamoto kubwa ilikuwa inanikabili ni namna gani ya kuinua mkoa wa Kagera kwenye maendeleo," alisema Dk. Magufuli na kuongeza:

"Ndiyo maana nikateua mawaziri watatu, Atashasta Nditiye ashughulikie ujenzi, Dk. Philip Mpango ashughulikie miradi ya nchi pamoja na Kigoma, Profesa Joyce Ndalichako ashughulikie elimu, lengo ni kuifanya Kigoma kupiga hatua kimaendeleo."

Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano, serikali imefanya mambo makubwa katika mkoa wa Kigoma ikiwamo kupeleka umeme, sekta ya elimu na mawasiliano.

Alisema lakini bado serikali haijamaliza kufanya shughuli za kimaendeleo katika mkoa huo, kwamba kuna mambo makubwa mazuri yatafanyika.

"Ninawahakikishia barabara kutoka Kibondo-Kasulu hii tutaikarabati kwa kiwango cha lami, leo nimeipita nimeiona na ninawaahidi nikirudi tena nitapita kwenye lami," alisema Dk. Magufuli.

Dk. Magufuli alisema kero zinazowakabili wananchi wa Kigoma anazifahamu ikiwamo mgogoro wa wachimbaji wadogo wa madini ya chokaa na wakala wa huduma za misitu, ambao wamekuwa wakivutana kuhusu uchimbaji wa madini hayo katika misitu.

Alisema pia anafahamu mgogoro wa mpaka baina ya kikosi cha JKT kikosi 895 na Mtabila.

Alisema pia kuna changamoto ya kutokukamilika kwa mradi wa REA unaotekelezwa na kampuni ya uhandisi ya CC wenye thamani ya Sh. bilioni 44 kupeleka umeme katika vijiji 22, uliopaswa kukamilika Oktoba, mwaka huu.

"Nataka nyie wabunge mtakaochaguliwa shughulikieni hili, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma umuite mkandarasi katika kamati ya ulinzi na usalama ahojiwe, hawezi kupewa pesa halafu achelewe kumaliza, Tanzania siyo ya kuchezewa," alisema na kuongeza:

"Ninaimani huyo mkandarasi ananisikia na kunielewa, pia ninataka Bodi ya Makandarasi wamuite huyo mkandarasi na kumuhoji."

Aidha, Dk. Magufuli alisema serikali imefanikiwa kudhibiti matukio ya ujambazi, utekaji, ulinzi na usalama katika mkoa wa Kigoma.

## HABARI KITAIFA

# NEC yakamilisha kupitia rufani za ubunge, udiwani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imekamilisha uchambuzi na kutoa uamuzi wa rufani za ubunge 153 na udiwani 393.

Kazi hiyo ilianza Septemba 8 hadi juzi jioni ambapo Tume ilichambua na kutoa uamuzi wa rufani hizo kati 557 za ubunge na udiwani zilizowasilishwa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Tume hiyo, Dk. Wilson Mahera, kazi hiyo ilikamilika juzi na kwa sasa inatengenezwa taarifa ya mwisho na kuwaandikia barua wagombea juu ya uamuzi wa NEC.

Alisema rufani hizo zimewasilishwa chini ya kifungu cha 40(6) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ambacho kinatoa fursa kwa wagombea wa ubunge kukata rufani wanapokuwa hawajaridhika na uamuzi wa wasimamizi wa uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa.

Alisema tume imechambua vielelezo, nyaraka na maelezo ya warufani na warufaniwa vilivyowasilishwa ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka kwa mujibu wa sheria na kanuni za uchaguzi.

Septemba 8, mwaka huu, NEC ilipitia rufani 55 za ubunge ambapo ilikubali 15 na kuwarejesha wagombea katika orodha ya wagombea huku ikikataa 15 za wagombea ambao hawakuteuliwa na kukataa rufani 25 za kupinga walioteuliwa.

Septemba 9, mwaka huu, zilichambuliwa na kutolewa uamuzi rufani 34 za ubunge, ambapo kati ya hizo 13 zilikubaliwa na wagombea kurejeshwa, rufani saba zilikataliwa za wagombea ambao hawakuteuliwa huku 14 za kupinga walioteuliwa zikikataliwa.

Septemba 10, ilitoa uamuzi wa rufani 67 ambapo kati ya hizo 22 za ubunge na 45 za udiwani.

Kwa upande wa ubunge, NEC ilikubali rufani 19 na kuwarejesha wagombea huku ikikataa rufani tatu za kupinga walioteuliwa.

Kwenye udiwani, tume hiyo ilikubali rufani 26 na kurejesha wagombea udiwani huku ikikataa rufani 16 za wagombea ambao hawakuteuliwa na rufani tatu za kupinga walioteuliwa.

Septemba 11, NEC ilipitia rufani 60 kati ya hizo mbili za ubunge na 58 za udiwani.

Katika rufani hizo, Moja ya ubunge ilikubaliwa mgombea kurejeshwa na moja kukataliwa ya mgombea ambaye uteuzi wake ulitenguliwa.

Pia rufani 34 za udiwani zilikubaliwa na wagombea kurejeshwa, huku 23 zikikataliwa za wagombea ambao hawakuteuliwa na moja ikikataliwa ya kupinga aliyeteuliwa.

Septemba 12, tume hiyo ilitoa uamuzi wa rufani 46 za udiwani ambapo kati ya hizo 24 zimekubaliwa na kurejesha wagombea, 13 za wagombea ambao hawakuteuliwa zimekataliwa huku tisa za kupinga walioteuliwa pia zikikataliwa.

Septemba 13, ilitoa uamuzi wa rufani 50 ambapo kati ya hizo nne ni za ubunge na 46 ni za udiwani ambapo za ubunge zote zimekataliwa, huku kwenye udiwani rufani 25 zilikubaliwa, rufani 12 za wagombea ambao hawakuteuliwa zilikataliwa na rufani tisa za kupinga wagombea udiwani walioteuliwa zimekataliwa.

Aidha, Septemba 14, rufani 49 za wagombea udiwani huku 24 zikikubaliwa na rufani 19 zimekataliwa za wagombea ambao hawakuteuliwa na zingine sita zilikataliwa za kupinga walioteuliwa.

Septemba 15, NEC ilitoa uamuzi wa rufani 67 ambapo kati ya hizo rufani tano ni za ubunge na 62 ni wagombea udiwani.

Katika rufani za ubunge, Tume ilikubali rufani tatu za wagombea ambao uteuzi wao ulitenguliwa na kukataa rufani mbili za wagombea ambao hawakuteuliwa.

Kuhusu rufani za udiwani, NEC ilikubali rufani 29, huku ikikataa rufani 23 za wagombea ambao hawakuteuliwa na 10 za kupinga wagombea udiwani walioteuliwa.

# Polisi wabainisha sababu kukamatwa msaidizi wa Membe

**Na Romana Mallya**

KAMANDA wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, amesema wanamshikilia, Jerome Luanda, msaidizi wa mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, kwa tuhuma ya utakatishaji fedha.

Juzi, Membe kupitia ukurasa wake wa Twitter aliandika kuwa msaidizi wake amechukuliwa na watu wasiojulikana, hivyo akatoa saa kadhaa ili kupatikana kwake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamanda Mambosasa alikiri Jeshi la Polisi kumshikilia msaidizi huyo wa mgombea wa ACT- Wazalendo.

"Mlinzi wa Membe kimsingi tunaye, tumemkamata na alikamatwa akitoka safarini akiwa na Membe mwenyewe. Amekamatwa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Hakukamatiwa mahali pa giza, amekamatwa mchana.

"Kuna watu wameanza kusema kuwa mara amekamatwa na watu wasiofahamika, mara nimezunguka vituo vyote vya polisi sijamwona. Ninamshangaa anayesema hivyo kwa sababu huwezi ukazunguka vituoni bila kuingia mahabusu kuangalia kama watuhumiwa hao wapo au hawapo."

Kamanda Mambosasa alisema Membe anayemsikia, hadhani kama anafahamu vituo vyote vya polisi. "Tunaofahamu ni sisi, na huyu nasema amekamatwa kwa ajili ya kuhojiwa kwa kosa la kutakatisha fedha. Ni suala la kuja halafu tumweleze ukweli wa jambo," alisema.

Kuhusu kwenda mahakamani, Kamanda Mambosasa alisema mpelelezi wa mkoa huo atakapokamilisha na kumkabidhi, atalipitia na kulipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kulitolea maelekezo.

Alipoulizwa kuhusu mtuhumiwa huyo yuko kituo gani cha polisi kwa sasa, alisema hawezi kueleza na kwamba kikubwa yuko mikono salama anahojiwa na anayetaka kujua yuko wapi anakaribishwa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUCHUKUA MAFUTA KUTOKA BANDARI ZA TANGA NA MTWARA**

Serikali ilianzisha matumizi ya Bandari ya Tanga ikiwa ni eneo la miundombinu la pili ya kupokelea bidhaa za mafuta baada ya Bandari ya Dar es Salaam. Pia Serikali ilianzisha matumizi ya Bandari ya Mtwara kama eneo la miundombinu ya tatu kwa ajili ya kupokea mafuta ili pamoja na mambo mengine, kupunguza gharama za kufanya biashara nchini. Kutokana na hatua hii, Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) na wadau wa biashara ya mafuta wamekuwa wakitumia bandari hizo tatu.

Hata hivyo, pamoja na juhudi nzuri za Serikali, EWURA imegundua kuwepo kwa baadhi ya wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara walioanza kununua mafuta kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kuyasafirisha kwa ajili ya matumizi katika mikoa hiyo. Pia EWURA imegundua kuwepo kwa wafanyabiashara wa Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi wanaochukua mafuta kutoka Bandari ya Dar es Salaam badala ya Bandari ya Mtwara. Hatua hii ovu imewaathiri wauzaji mafuta ya jumla wanaoingiza kupitia Bandari ya Tanga na Mtwara, ambapo pia inaathiri juhudi za Serikali za kupunguza gharama za kufanya biashara kumnufaisha mlaji wa mwisho.

Hivyo basi, EWURA inatoa **Agizo** kuwa mafuta yote yatakayotumika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara lazima yawe ni yale yaliyopitia Bandari ya Tanga na kwa mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi, lazima yawe ni yale yaliyopitia Bandari ya Mtwara na si vinginevyo.

**Mtu yeyote atayekiuka Agizo hili atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa kifungu cha 238 cha sheria ya Petroli, Sura ya 392, na akipatikana na hatia adhabu yake ni faini si chini ya shilingi milioni 100 au kifungo cha miaka si chini ya 10 au vyote.**

EWURA inafuatilia kwa karibu hali ya upatikanaji wa mafuta nchini ili kuhakikisha maslahi ya wadau wote wakiwemo watumiaji, makampuni ya mafuta na serikali yanalindwa.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

215904102

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P. 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-3, Nukushi: +255 26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya kifungu Na.19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 17 (4) ya Kanuni za Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations), Gazeti la Serikali Toleo Na. 380 la 2018)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| **Jina la awali la kituo** | : | Dennis Shoo Trust Oil Filling Station |
| **Nambari ya Leseni** | : | PRL-2019-110 |
| **Mahali Kituo kilipo** | : | Kiwanja No. 2439, Kitalu "M" Eneo la Chanika Buyuni, Wilaya ya Ilala |
| **Jina linalopendekezwa** | : | Sultanate Energy Company Limited |
| **Mmiliki wa awali** | : | Dennis Richard Swai |
| **Mmiliki mpya** | : | Sultanate Energy Company Limited |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Imetolewa na**
**MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

215906302

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P. 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-3, Nukushi: +255 26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz

# Jela miaka 30 kumbaka mtoto wake

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela mkazi wa Mtaa wa Kimpungua, Manispaa ya Singida, Hamisi Mtanda (37) kwa kosa la ubakaji.

Mtanda amehukumiwa kifungo hicho baada ya mahakama kumtia hatiani kwa kosa la kufanya mapenzi na mtoto wake wa kike, mwenye umri wa miaka 11.

Ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Elizabeth Barabara, kwamba mshtakiwa alianza kufanya mapenzi na mtoto wake huyo (jina linahifadhiwa) kuanzia Julai, mwaka jana, kwa kumchokonoa kwa vidole baada ya kutengana na mama wa mtoto huyo.

Mwanasheria huyo alidai kuwa mshtakiwa alitengana na mke wake, ambaye ni mama mzazi wa mtoto, Modesta Mshana na hivi sasa anaishi mkoani Dar-es-Salaam na alikwenda kumchukua mtoto huyo akiwa na umri wa miaka sita na kuanza kuishi naye.

Barabara alidai kuwa katika kipindi chote hicho, mshtakiwa huyo kabla ya kuanza kumwingilia kimwili mtoto ambaye ni mwanafunzi (jina la shule linahifadhiwa), alikuwa akimnyemelea usiku akiwa amelala.

Alidai kuwa mshtakiwa baada ya kuona sehemu za siri za mtoto zimetanuka, ndipo alipoanza kumwingilia kimwili na wakati akifanya unyama huo, mtoto alikuwa akipiga kelele za kuomba msaada bila mafanikio kutokana na maumivu aliyokuwa akiyapata.

Mwanasheria huyo alidai kuwa, kutokana na mshtakiwa kukana shtaka la kutenda kosa hilo, upande wa Jamuhuri ulipeleka mashahidi sita, akiwamo daktari ambaye alithibitisha bila kuacha shaka yoyote kwamba mshtakiwa ndiye aliyemwingilia mtoto huyo.

Kutokana na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, mahakama ilijiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa mshtakiwa huyo ndiye aliyemfanyia unyama huo mtoto wa kumzaa mwenyewe.

Kabla ya kutolewa adhabu, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea kwa kudai kuwa hakufanya unyama huo bali mtoto huyo alikuwa amefanya vitendo vya ngono na mwalimu, bila kumtaja ni mwalimu yupi.

Akitoa hukumu, Hakimu Mkazi Mwandamizi Robert Oguda, alisema anamhukumu mshtakiwa kifungo cha miaka 30 jela, ili iwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama za mshtakiwa huyo.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Mazingira (DAWASA) wakizibua chemba iliyokuwa imeziba eneo la DDC Mlimani mtaa wa Mlalakuwa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: FLORIDA RAYMOND**

# TRA yawapa wafanyabiashara elimu ya kodi

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), katika kuhakikisha wafanyabiashara wanalipa kodi na tozo nyingine imeamua kuwafikia na kutoa elimu kuhusu mabadiliko ya sheria za kodi.

Katika mada yake aliyoitoa jana kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mtwara, Ofisa Mkuu Usimamizi wa Kodi TRA, Rose Mahendeka, alisema serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 imefanya marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwamo kubadilisha baadhi ya kodi, tozo na ada.

Alisema serikali imerekebisha sheria zingine zinazohusu ukusanyaji na usimamiaji wa mapato yatokanayo na kodi na yasiyo ya kodi.

"Marekebisho haya yanalenga kusaidia katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hususani sekta ya kilimo, viwanda, kuongeza ajira na mapato ya serikali," alisema.

Mahendeka alisema TRA inatoa elimu kwa wafanyabiashara na wadau wengine kwa kuwa mabadiliko hayo yanawahusu moja kwa moja.

"Ni wajibu wetu kuwapa elimu hii ili muweze kuelewa na kulipa kodi kwa wakati, TRA inatoa elimu ya mabadiliko ya sheria za kodi kwa wadau mkiwamo nyinyi, wenye viwanda, kilimo na shughuli au huduma zingine zinazotakiwa kulipa kodi," alisema.

Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) mkoani humo, Swallah Swallah, alisema elimu hiyo ni muhimu kwa wafanyabiashara kwa kuwa zinaongeza uelewa wa masuala ya kodi.

Mfanyabiashara, Bharat Dhokia, alisema wanapoelimishwa inawafanya wajue wajibu wao wa kulipa kodi kwa hiari.

Naye mfanyabiashara Ezekiel Akida aliishukuru TRA kwa kuwafungua macho kwa kuwafundisha vitu ambavyo walikuwa hawavijui.

# Majaliwa awapiga kijembe wapinzani

**Na Happy Severine,** SIMIYU

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wananchi wa Mkoa wa Simiyu na wanachama wa vyama vingine vya upinzani kutoogopa kuwapigia kura wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa kuwa chama hicho ndicho pekee kilicho imara na kinachotekeleza ilani yake kwa vitendo.

Kadhalika amesema ndani ya kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa awamu ya tano, chama hicho kimewaletea wananchi maendeleo makubwa katika sekta zote hivyo na kuwataka waendelee kukiamini kwa kukipigia tena kura ili wafanye zaidi ya walipofanya.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya mgombea ubunge wa Jimbo la Bariadi uliofanyika katika Shule ya Msingi Nkololo, wilayani humo.

Aliwataka wananchi wote wa Mkoa wa Simiyu bila kujali vyama vyao kuwachagua viongozi wa CCM na waepuke kuchanganya viongozi wa chama hicho na vyama vingine kwa kuwa kufanya hivyo watashindwa kuwa kitu kimoja wakati wa utekelezaji wa ilani yao ya chama.

Alisema CCM kina benki ya viongozi wa kutosha ambao wanaweza kufanya kazi ipasavyo kwa kuzingatia ilani yao hivyo ni vyema wakatumia haki yao ya msingi na kikatiba kwa kuchagua viongozi bora watakaotatua kero na changamoto za wananchi.

Mgombea ubunge Jimbo la Bariadi, mkoani Simiyu, Andrea Kundo, aliwaomba wananchi wa jimbo hilo wamchague ili aweze kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Mhandisi Kundo alisema endapo atachaguliwa ataanza na utatuzi wa uhaba wa watumishi katika sekta ya afya, miundombinu ya barabara na uvamizi wa tembo katika mashamba na makazi ya wananchi.

"Natambua kazi kubwa iliyofanywa na serikali ya awamu ya tano pamoja na watangulizi wangu ndani ya Jimbo la Bariadi ila nami niwahakikishie wananchi ushirikiano wa karibu katika kuendeleza miradi iliyoachwa na mtangulizi wangu, Andrea Chenge," alisema.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Simiyu, Enock Yakobo, aliwataka wagombea wote wa CCM watakapochaguliwa kutimiza ahadi zao ili chama hicho kizidi kuaminiwa.

# IPP yaibuka na wateule 10 tuzo za EJAT

**Romana Mallya na Frank Maxmillian** (TUDARCO)

WAANDISHI wa habari 10 wa Kampuni ya IPP Media, wameteuliwa kuwania tuzo za umahiri wa uandishi wa habari (EJAT) 2019 zilizoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Wateule hao ni Mhariri wa Habari wa Nipashe, Sanula Athanas na waandishi waandamizi Gwamaka Alipipi, Ashton Balaigwa na Marko Maduhu na Rahma Suleiman (Nipashe).

Wengine ni James Kandoya, Crispin Samson (Guardian), Muhidin Msamba (mchora vibonzo Guardian), Abdul Kingo (mchora vibonzo Nipashe) na marehemu Agnes Almasy (ITV).

Akitangaza majina ya wateule hao jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT 2019, Kajubi Mukajanga, alisema jumla ya wateule katika tuzo za EJAT 2019 ni 56 kutoka vyombo mbalimbali vya habari.

Alisema kati yao, 25 ni kutoka kwenye magazeti, 21 redio, 10 runinga, wanawake ni 24 na wanaume 32.

Alisema washindi wa tuzo hizo watajulikana rasmi Jumatatu ijayo, katika kilele cha tuzo za EJAT zitakazofanyika mkoani Tanga na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa huo, Martin Shigella.

Alisema kamati ilipokea jumla ya kazi 450 na kati ya hizo, 192 ni kutoka magazeti wakati wanahabari wa redio na runinga waliwasilisha kazi 250 na vyombo vya habari vya mitandaoni vikipeleka kazi nane.

Alitaja makundi yatakayoshindaniwa kuwa ni 21, baadhi yake ni tuzo ya kuripoti biashara, uchumi na fedha, tuzo ya utamaduni na michezo, tuzo ya elimu na tuzo ya kuripoti utalii na uhifadhi.

Makundi mengine ni tuzo ya kuripoti habari za uchunguzi, habari za data, haki za binadamu na utawala bora, mpiga picha bora, mchora vibonzo bora na habari za jinsia.

Tuzo za kuripoti habari za wazee, watoto, usimamizi wa mafuta, gesi na uchimbaji madini na afya ya uzazi.

Mengine ni ubunifu wa maendeleo ya binadamu, athari za kemikali kwa afya na mazingira, usalama barabarani, hedhi salama na tuzo ya wazi.

Mukajanga alisema wateule hao wamepatikana baada ya jopo la majaji kukaa Septemba 8 na kupitia kazi zilizowasilishwa, ambazo zimegawanywa katika makundi 21.

Alisema jopo la majaji liliongozwa na waandishi nguli Pudenciana Temba, Mohammed Kissengo, Imane Duwe, Khalfan Said, Mkubwa Ally na Pili Mtambalike ambaye alikuwa Katibu.

Alisema wajumbe wa kamati ya maandalizi ni MCT, Mwenyekiti ni Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF) na Taasisi ya Habari ya Kusini mwa Afrika tawi la Tanzania (MISA-Tan).

Wengine ni Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT), HakiElimu, ANSAF, Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) na SIKIKA.

Katika hatua nyingine, Mukajanga aliwaasa wamiliki wa vyombo vya habari kukumbuka kuwa pamoja na umuhimu wa vipaji, waelewe kuwa watangazaji na waandishi wao wanahitaji kuwa na stadi za taaluma.

"Baraza limebaini mwenendo unaokua wa kukiuka maadili kwa baadhi ya vyombo vya habari. Ukiukwaji huu wa misingi ya taaluma unaonekana katika matumizi ya lugha zisizozingatia maadili na utamaduni wa Mtanzania."

"Mijadala ya wazi na isiyo na chembe ya staha ya masuala ya ngono, kuripoti masuala ya uchaguzi pasipo kuzingatia msingi wa haki na ulinganifu na kuchapisha tuhuma, bila kufanya jitihada za kuzithibitisha au kutoa nafasi ya mtuhumiwa kujibu."



Mkurugenzi wa Sera Taifa wa Chama cha Sauti ya Umma (SAU), ambaye ni mgombea ubunge Jimbo la Kibamba jijini Dar es Salaam, Kunje Ngambale Mwiru, akihutubia mkutano wa kampeni wa chama hicho, katika Soko la Feri juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wagonjwa selimundu waiangukia serikali

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha wagonjwa wa selimundu, kimeiomba serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuwapatia huduma za vipimo, dawa pamoja na kumuona daktari, kupitia mfuko huo.

Mwenyekiti wa chama hicho, Arafa Said, alisema wagonjwa hao hulazimika kulipia huduma hizo kwa fedha taslimu, licha ya baadhi yao kuwa na bima za afya.

Arafa aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa kliniki ya wagonjwa wa selimundu na magonjwa ya moyo 'Sickle cell Cardiac Clinic' itakayoshirikisha Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Alisema hiyo ni changamoto kubwa kwao, hususani katika matibabu pamoja na kliniki wanazohudhuria kila mwezi na kwamba gharama nyingine haziruhusiwi na mfuko huo.

"Ongezeko katika ada ya kumuona daktari kliniki kila mwezi, vipimo pamoja na dawa, inawafanya wagonjwa wa selimundu kupata madhara ya magonjwa yanayoambatana na ugonjwa huo.

"Asilimia kubwa ya wagonjwa wa selimundu hawamudi kugharamikia gharama za matibabu, kifurushi cha mtoto kina ukomo katika kumpatia mgonjwa, kwani baadhi ya dawa hawapatiwi katika kifurushi cha watoto," alisema Arafa.

Pia alisema ukosefu wa huduma za wagonjwa hao hususan kipimo cha moyo kwa baadhi ya hospitali, kunawafanya kukosa kipimo hicho muhimu cha moyo ambacho kinashauriwa kipimwe angalau mara moja kwa mwaka.

"Nampongeza Rais John Magufuli kwa kuboresha huduma za afya nchini, lakini tuna changamoto... tunaishi na selimundu. Vipimo vya kugundua iwapo una selimundu ni hapa Muhimbili au tawi lake, hii inafanya kuwe na gharama kubwa."

Awali, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Chuo cha MUHAS, Mkuu wa Utafiti katika chuo hicho katika Programu ya Selimundu, Dk. Paschal Ruggajo, alisema upo uwezekano mkubwa, wanaougua selimundu, kuugua magonjwa ya moyo.

Alisema ipo haja ya ushirikiano wa kufanya utafiti kwa pamoja na kumpatia matibabu mgonjwa hususani wanaougua selimundu. Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alisema mgonjwa wa selimundu anaweza kuzaliwa nao na kuna uwezekano pia wa kupata ugonjwa wa moyo, hivyo kliniki hiyo itasaidia tiba ya pamoja.

"Kituo kiwe cha pamoja 'one stop centre' mtu akija na selimundu, shida ya moyo atibiwe mahala pamoja. Tupo katika 'sickle cell cardiac program' ambayo itasaidia mpango huu katika matibabu," alisema Prof. Janabi.

"Tulijadili kuanzisha kliniki hii ya pamoja, ili kuhudumia mtoto na Mtanzania. JKCI tunatumia Sh. bilioni 1.3 hadi 1.5 kwa mwaka, kwa ajili ya msamaha, yaani Sh. milioni 120 hadi 150 kwa mwezi."

Prof. Janabi alisema ushirikiano huo na MUHAS katika mpango wa kutoa huduma kwa wagonjwa wa selimundu, itaboresha huduma hizo.

# TIC yajipanga kuibua fursa kupitia SGR

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi, amekutana na wadau kuangalia namna ya kuibua fursa za kiuchumi pembezoni mwa mradi wa reli ya kisasa (SGR) pindi itakapoanza.

Wadau hao ni pamoja na Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Akizungumza kwenye kikao hicho kilichofanyika jijini Dodoma juzi, Dk. Kazi alisema wamekutana, ili kuandaa mpango wa kuibua fursa za uwekezaji zinazotokana na kuwapo kwa mradi huo.

Dk. Kazi alisema TIC imeona ni vyema kuibua fursa au shughuli za kiuchumi zinazotakiwa kufanyika katika maeneo ya pembezoni mwa reli.

Alisema hiyo itasaidia kuleta ufanisi na tija kwa reli na jamii iliyopo pembezoni.

"Uwapo wa reli hii ni mojawapo ya maboresho ya mazingira ya uwekezaji kwenye miundombinu yanayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli," alisema.

Dk. Kazi alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji Na. 26 ya mwaka 1997, miongoni mwa majukumu ya TIC ni kuibua, kuhamasisha na kunadi fursa za uwekekezaji nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema wako tayari kutoa ushirikiano, ili kufanikisha malengo ya kuhakikisha reli hiyo inaleta manufaa zaidi kwa jamii iliyopo pembezoni mwa reli.

Naye Kamishna Mkuu wa TRA, Dk. Edwin Mhede, alisema mpango huo unapaswa kushirikisha sekta binafsi na wadau wengi wa sekta binafsi na serikali.

"Mpango huu ni mzuri wenye nia ya kuifanya reli yetu isiishie kubeba mizigo na abiria tu bali iende sambamba na faida zingine za kiuchumi, uwekezaji pamoja na elimu kwa mlipakodi, ili kukusanya mapato ya serikali bila kuwaletea usumbufu wawekezaji," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kasi ya hamasa ya kupiga kura muhimu

**WATANZANIA** wanatarajia kufanya uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu wa kuwachagua rais, wabunge na udiwani.

Upigaji kura utafanyika baada ya kukamilika kwa mchakato muhimu wa kampeni zinazoendelea kwa sasa katika maeneo yote ya nchi yetu, kwa ajili ya vyama vya siasa na wagombea wake kuwashawishi wananchi wawachague kuiongoza nchi kwa kipindi cha miaka mitano. Tangu kampeni hizo zilipoanza, wagombea wa ubunge wamekuwa wakijinadi katika majimbo yao pamoja na madiwani katika kata zao, huku wa urais wakipita nchi nzima kueleza ilani, sera, mikakati yao na ya vyama vyao katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Hata hivyo, kwa baadhi ya walioomba uteuzi wa kugombea udiwani na ubunge na kuwekewa mapingamizi katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) rufani zao zinaendelea kushughulikiwa, na kwa mujibu wa tume, zoezi hilo lilitarajia kukamilika wakati woote. Kwa watakaopitishwa kugombea nao watawajibika kufanya kampeni za kujinadi kwa kipindi cha takribani mwezi mmoja na siku kadhaa ili wananchi wawafahamu na kujua nini hasa wanatarajia kuwafanyia.

Kimsingi, mchakato wa kampeni ulipaswa kwenda sambamba na elimu kwa wapigakura, haswa kuhamasishwa kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura, hivyo kutimiza haki yao ya msingi ya kikatiba ya kuwachagua viongozi wanaowataka.

Tunasema hivyo kwa sababu wananchi wanapaswa kutambua umuhimu wa kushiriki kupiga kura kwa wingi kama wanavyoshiriki kwenye kampeni, japo taratibu za kwenda kwenye kampeni ni tofauti na zile za kupiga kura.

Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 kifungu cha 4C imeipa NEC mamlaka ya kutoa elimu ya mpigakura nchi nzima, kuratibu na kusimamia Taasisi, Asasi na watu wanaotaka kutoa elimu ya mpigakura. Kwa matakwa hayo ya sheria, NEC hutoa eimu ya mpigakura kwa kushirikiana na asasi za kiraia katika kutoa elimu hiyo katika kuelimisha umma kuhusu mchakato wa uchaguzi pamoja na kutoa vibali kwa Asasi za kiraia kushiriki kutoa elimu ya mpigakura. NEC imejiwekea utaratibu wa kuzialika asasi hizo zinazokusudia kutoa elimu hiyo, ambapo huwasilisha maombi na zana zao za elimu ya mpigakura ili kupitia na kuidhinisha pamoja na nyenzo zote za elimu hiyo.

Pia ni jukumu la NEC kupitia na kuidhinisha mipango (program) yote iliyoainishwa na wadau wa utoaji wa elimu ya mpigakura pamoja na kufuatilia na kuratibu mpango wa utaoaji wa elimu ya mpigakura ili kuhakikisha kwamba inatolewa kwa umakini, usahihi bila kupotosha wananchi na zinawafikia walengwa wote waliokusudiwa.


Kwa mwaka huu 2020 asasi zilizopitishwa kutoa elimu ni 245 ambapo kati ya hizo 97 zitashiriki katika uangalizi wakati wa kupiga kura. Hata hivyo, tumeshuhudia kasi ndogo ya uhamasishaji wa kupiga kura, hali ambayo inatia shaka kama umuhimu wa elimu hiyo unapewa uzito unaostahili kwa jamii.

Utoaji wa elimu hauna budi kutumia mbinu za aina mbalimbali katika kuhakikisha elimu inawafikia walengwa na lengo lililokusudiwa linafanikiwa.

Kuna baadhi ya asasi ambazo zimeanza kutoa elimu kwa njia mbalimbali ikiwamo mitandao ya kijamii, lakini inapaswa kufuatilia kwa karibu kama ujumbe wao umewafikia walengwa, je, umesomwa au kuangaliwa na watu wangapi.

Tunaona kuwa muda wa uchaguzi uliobakia ni mfupi, hivyo ni mwafaka kwa wahusika kuzidisha kazi ya utoaji elimu ya mpigakura kuhakikisha kuwa siku ya uchaguzi anajitokeza kituoni na kupiga kura. Bila kuongeza kasi ya elimu hiyo, inaweza kutokea wachache wakapiga kura na kuwachagulia viongozi Watanzania walio wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# Wajasiriamali pasueni vichwa kufaidika bomba la mafuta

**FURSA** za kiuchumi zinazonukia katika mradi wa kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanga (EACOP), ni jambo la kuchangamkia kiuwekezaji na kuhakikisha kuwa zinaleta maisha bora kwa majirani wa bomba hilo.

Katika biashara au ulipo mradi wa maendeleo wowote wakazi au majirani wa maeneo husika wananufaika na ikibidi wanabadilika kwa kubuni mbinu mbalimbali za kujiingiza kwenye biashara zenye tija.

Watanzania wanatakiwa kuamka kwa vile kuna ulegevu fulanI unaoonekana hasa kwenye miundombinu. Licha ya kuwapo na barabara nyingi nchini, wengi hawachangamkii fursa na kuwekeza pembeni ya barabara hizo, mathalani kutoka Arusha mpaka Dar.

Wajasiriamali pamoja na halmashauri za wilaya na mikoa hazijaanza kuliona hilo, lakini wakati umefika waanze kuamka.

Kwa upande wa bomba la Hoima wakati umefika wajasiriamali kama mama na babalishe, wenye nyumba za wageni, hoteli , zahanati, vituo vya afya pamoja na wamiliki wa usafiri kutumia fursa hiyo ipasavyo.

Ninasema hili baada ya Tanzania na Uganda kutiliana saini mkataba wa ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi mkoani Tanga kwenye bandari.

Marais John Magufuli na Yoweri Museveni wa Uganda hivi karibuni waliwekeana saini kukubaliana kufunguliwa rasmi milango ya ujenzi na kutangaza mwanzo wa fursa mbalimbali za kiuchumi hii ni kazi inayokuja baada ya wakuu hao wa nchi kuweka jiwe la msingi mwaka 2017.

Pia imebainika kwamba Tanzania itapata asilimia 60 ya mapato ya biashara hiyo ya mafuta huku Uganda ikipata asilimia 40.

Mradi huo mkubwa Afrika Mashariki unakadiriwa kuwa na urefu wa kilomita 1,445 na kusafirisha mapipa 216,000 kwa siku, na kila pipa litalipiwa Dola za Kimarekani 12.2.

Bomba hilo kwa upande wa Tanzania litasimamiwa na Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (TPDC) litagharimu Sh. bilioni 3.5.

Inakadiriwa maeneo mengi Watanzania wanaweza kufungua fursa za kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali hasa kwenye kata 132, vitongoji 1,112, vijiji zaidi ya 186 pamoja na wilaya 24 kote huko wakijihusisha na shughuli mbalimbali.

Pia kupitia mradi huo kutakuwa na vituo 14 na wamiliki wa ardhi watakaoguswa na mradi huo watalipwa fidia ya bilioni 9.9.

Katika maeneo hayo unakopita mradi huo watakuwapo wataalamu wa ujenzi, wahandisi, washauri pamoja na vibarua mbalimbali wanaohitaji kupata huduma tofauti.

Kwa vyovyote vile kutahitaji malazi, chakula, huduma za afya, shule, burudani na mahitaji ya urembo zikiwamo saluni za wanaume na wanawake wakati wote wa kipindi cha utekelezaji mradi huo.

Inamaanisha kuwa Watanzania wanapaswa kusoma alama za nyakati na kuacha kufanya biashara za mazoea yaani kuingiza kipato kidogo cha kusaidia familia kula pekee, badala yake waamke na kufanya uwekezaji makini wenye manufaa makubwa.

Kwa wafanyabiashara wabunifu na wazoefu wataelewa kwamba ni ni fursa yao, kukua kiuchumi kwa kuwekeza miradi mbalimbali ili kutoka hatua moja hadi nyingine.

Kwa wafanyabiasahara ndogondogo wasiohitaji mtaji mkubwa .


Wanaouza vyakula wachangamkie biashara ya kulisha chakula kwa kuwa takribani Watanzania 10,000 watahusika katika kazi ya kujenga bomba hilo.

Maisha ya wakazi wa maeneo hayo yanaweza kubadilika na kuinuka kiuchumi kwa kuongeza kipato iwapo watatumia fursa nyingi za kibiashara pamoja wakiboresha maisha yao na kuhudumia ipasavyo familia.

Kwa wakulima ni wakati wa kulima mazao yenye tija kwa kuwekeza kwenye uzalishaji mkubwa wa mazao, ili mahitaji yakiongezeka kwa walaji iwe fursa kwao.

Bomba la mafuta ni uwekezaji wa kiuchumi kwa Watanzania ambao wana jicho la kuona fursa na kuitumia ili kubadili maisha na kuwa na maendeleo endelevu.

BURIANI



# Jaji Bomani atakumbukwa usimamizi tasnia ya habari

Na Habbi Gunze

SIKU ya kwanza ya wiki hii yaani Jumatatu 14, Septemba, 2020 imekuwa ya taarifa za masikitiko na huzuni kubwa Tanzania. Kwanza, tumepoteza wanafunzi 10 wa Shule ya Sekondari ya Bweni Kyerwa, Kagera kuteketea kwa moto baada ya bweni lao kuungua.

Pili wanahabari wa tasnia ya utangazaji waliungana na Watanzania kuomboleza na kuzika mwili wa marehemu Jaji Mark Dahni Bomani (pichani), katika makaburi ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Marehemu Jaji Bomani, amefahamika zaidi kwa kuwa mwanasheria mwenye umri mdogo zaidi (miaka 33), aliyeshika wadhifa wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kwanza Mtanzania mwaka 1965, miaka mitano tu baada ya Tanzania kupata uhuru mwaka 1961 wakati ambapo nchi ilikuwa na wataalamu wachache wazalendo katika fani zote ikiwamo sheria.

Kubwa ambalo mimi nataka kumwelezea Jaji Bomani ni kuhusu jambo ambalo halifahamiki sana au limesahauliwa na jamii katika baadhi ya michango mikubwa ambayo Jaji Bomani alitoa. Jaji Bomani alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utangazaji (TBC) kuanzia mwaka 1993 baada ya serikali kutunga Sheria ya Huduma za Utangazaji Na 6 ya mwaka 1993 (The Broadcasting Services Act no 6 of 1993).

Jaji Bomani alisimamia uanzishwaji wa Sekretariati ya Tume ya Utangazaji baada ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti na Rais Ali Hassan Mwinyi.

Sekretariati ya Tume Utangazaji ilikuwa imekamilika baada ya kuteuliwa kwa Habbi Gunze, (MA Journ) mwaka 1995 kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu ambaye alifahamika rasmi kwa cheo cha Msajili wa Tume ya Utangazaji (Registrar of the Tanzania Broadcasting Commision).

Tume ilianza na watumishi 10 katika idara za Utawala na Fedha, Uhandisi na Maudhui. Kuwapo kwa Sekretarieti ya Tume ya Utangazaji kulimfanya Jaji Bomani atembee kifua mbele kwa vile Tume ilianza kuwa na uwezo wa kutoa leseni za huduma ya utangazaji baada ya sekretarieti kuandaa taratibu zote za utoaji wa leseni za utangazaji kwa njia ya Radio, Televisheni na Kebo (Cable transmission).

Kwa kupitia uamuzi wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 1995 vituo vyote vya utangazaji vya watu binafsi viliruhusiwa kurusha matangazo kwa eneo lisilozidi asilimia 25 ya eneo la Tanzania.

TBC waliandaa leseni za utangazaji kwa kuzingatia maelekezo hayo ya serikali.

Hadi kufikia mwaka 2000 kulikuwa na vituo 14 vya radio vyenye leseni. Kati ya vituo hivyo, vituo anzilishi vya kwanza kupewa leseni vilikuwa ni Radio Sauti ya Injili , Moshi, Radio One, Dar es Salaam, Radio Free Africa, Mwanza na Radio Tanzania Dar es Salaam ambayo ilikuwa inafanyakazi ya kuhabarisha, kutaarifu na kuburudisha tangu mwaka 1951.

Tevisheni zilizopewa leseni ni Cable Entertainment Network (CEN), Coastal Television Network (CTN), Dar es Salaam Television (DTV), Independent Television (ITV), Sokoine University of Agriculture (SUA tv) na Abood Television (ATV).

Mafanikio tunayoona sasa hivi ya kukua kwa sekta ya utangazaji nchini, misingi yake iliwekwa na Jaji Mark Bomani na timu yake ndogo ya Sekretariati. Misingi hiyo ni pamoja na staili yake ya uongozi na usimamizi wa Tume ambayo ilikuwa shirikishi, imara, madhubuti na elekezi.

Jaji Bomani alihakikisha usimamizi na udhibiti wa tasnia ya utangazaji unaongozwa na sheria, kanuni na taratibu za tasnia ambalo ndiyo jiwe la pembeni lililoimarisha utangazaji nchini.

Sasa hivi tunajivunia kuwa na radio 183 na televisheni 42 na watoa huduma za maudhui ya kulipia kwa vifurushi 3 huduma za mitandao ya jamii kwa mfumo wa radio na televisheni ziko lukuki nchini.

Jaji Bomani hakuvumilia andiko lolote linalowasilishwa na Sekretariati kwenye vikao vya Bodi ya TBC ambalo halikuwa sahihi na kamilifu.

Sekretariati ilipata kujifunza toka kwa uelekezi kamilifu wa Jaji Bomani wa namna ya kuandaa makabrasha ya mikutano na uwasilishaji wake kwa namna ambayo kila mjumbe wa bodi alielewa.

Wakati wa mikutano, Jaji Bomani alichambua kila hoja inayowalishwa mezani na sekretarieti na kila mchango wa mjumbe wa bodi na hatimaye kuishawishi Bodi kuchukua maamuzi sahihi.

Wakati wa kujadili na kuwahoji waombaji wa leseni za huduma ya utangazaji, Jaji Bomani aliyekuwa na umri wa miaka 68, mwaka 2000 alikuwa hachoki hata kama vikao viliendelea hadi saa mbili usiku. Alishirikiana na wajumbe kuhakikisha kuwa kazi iliyo mbele yao inaisha kikamilifu.

Mimi mwenyewe nitamkumbuka Jaji Bomani kuwa mtu wa masaada sana kwangu kwa vile niliingia TBC na uzoefu wangu wa uandishi wa habari na uongozi, lakini nilikuwa sijawahi kufanya kazi ya udhibiti na usimamizi wa huduma ya utangazaji kwa vile ndiyo ilikuwa ni taaluma mpya enzi hizo.

Jaji Bomani hali akitambua hilo, alielekeza Sekretariati ya Tume kuandaa mafunzo ya udhibiti na usimamizi wa huduma za utangazaji ndani na nje ya nchi. Nakumbuka safari ya kwanza ya mafunzo nje ya nchi ilikuwa Marekani kwenye chuo cha United States Telecommunications Training Institute (USTTI), jijini Washington, mwaka 1998 na Commonwealth Broadcasting Association (CBA), London mwaka 2001 ambapo tulifundishwa na wabobezi wa udhibiti na usimamizi wa huduma za utangazaji ikiwamo mbinu za utoaji leseni na mbinu za udhibiti na usimamizi wa maudhui hasa maudhui hasi na yanayohatarisha usalama wa taifa na yanayodhalilisha wanawake na watoto.

Watumishi walijifunza namna bora ya kupanga masafa ya utangazaji ili kutoa huduma za utangazaji sawia kwa jamii zote mjini hadi vijijini na kuangalia mizania ya huduma hiyo kwa nchi nzima.

Watumishi waliporudi Jaji Bomani alifurahi sana kwa vile aliona kiwango cha kufanyakazi kimeongezeka na huduma za utangazaji zikawa zinaendeshwa ipasavyo. Makosa madogo ya watangazaji kwenye redio hewani na televisheni yalidhibitiwa na malalamiko ya wananchi kuhusu huduma hafifu hayakuwapo isipokuwa malalamiko yalikuwa ni kutaka serikali ifungue milango zaidi kwa vituo binafsi viweze kutangaza nchi nzima kutoka kwenye ukomo wa kutangaza kwenye eneo la asilimia 25 tu ya Tanzania nzima.

Miaka ya 2000 sekta ya utangazaji ilikuwa imeendelea sana huko bara la Ulaya na Marekani na hata Asia. Majaribio ya kutangaza kwa mfumo wa dijitali yaliishaanza Uingereza, Ujerumani na Japan. Shirika la Mawasiliano la Kimataifa (ITU), tayari liliishaanza kuzungumza namna ya kubadilisha mfumo kutoka utangazaji wa analojia hadi digitali.

Jaji Bomani alilijua hilo na akaagiza sekretariati ianze kulifanyia uchunguzi na kushiriki mikutano yote ya ITU kwa kushirikiana na Tume ya Mawasilano nchini (TCC). Kulikuwa tayari teknolojia ya mawasiliano ya simu inaingiliana na teknolojia ya huduma za utangazaji.

Mawasilino ya simu yalikuwa na ongezeko la hitaji la masafa kwa sababu huduma za simu miaka ya 2000 iliishahama kutumia teknolojia ya analojia na kuhamia mfumo wa dijitali kiasi kwamba huduma za simu zilihitaji upanuzi ili zienee zaidi kwa wananchi hadi vijijini. Njia madhubuti ya kufanikiwa ilikuwa ni kuchukua sehemu ya masafa ya utangazaji ambayo yalikuwa hayatumiki yakisubiri upanuzi wa huduma za utangazaji kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya dijitali.

Kasi ya kukua kwa teknolojia na huduma za simu zilifanya sekta ya utangazaji kubaki nyuma kwa sababu ilikuwa inatumia mfumo wa teknolojia ya analojia ambayo ilifikia ukomo wa kupanua huduma.

Mwingiliano wa teknolojia katika huduma za mawasiliano ya simu na utangazaji ni sababu ya msingi sana iliyoashiria serikali kuangalia upya kama huduma za udhibiti na usimamizi wa mawasiliano na utangazaji ziendelee kutolewa hivyo zilivyo au ziunganishwe.

Busara ilitumika kwa kuangalia masilahi mapana ya taifa na kuunganisha TBC na TCC ili kuwa na chombo kimoja cha udhibiti na usimamizi wa mawasiliano, utangazaji na huduma za posta.

Baada ya kuunganisha TBC na TCC mwaka 2003, na kuunda Tanzania Communications Regulatory Authority (TCRA) huduma ya Jaji Bomani kama Mwenyekiti wa TBC ilikoma.

Wanahabari wa tasnia ya utangazaji watamkumbuka Jaji Bomani kama kiongozi shupavu na madhubuti mwanzilishi wa huduma za udhibiti na usimamizi wa huduma utangazaji nchini ambaye aliasisi upanuzi wa huduma ya utangazaji kwa kushirikisha sekta binafsi katika kuwekeza kwenye vyombo vya utangazaji tunavyoviona hivi leo na kuvisikia vikirindima hewani.

**Bwana alitoa Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe. Amina**

# Wazazi wafundwa malezi ya watoto

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

OFISA Elimu wa Wilaya ya Mkuranga, Benjamin Majoya, amewataka wazazi na walezi kuwa karibu na watoto wao na kuwafuatilia mienendo yao, ili kuwaepusha kwenda kinyume cha maadili na kupoteza dira ya maisha.

Majoya alitoa wito huo, juzi alipokuwa katika mahafali ya Shule ya Sekondari Ujenzi, Mkuranga mkoani Pwani. Alisema kitendo cha kuwa karibu na watoto kitawafanya wakue wakiwa katika maadili mema ya Kitanzania na kuwafanya watimize ndoto za maisha yao.

Alisema wazazi wanatakiwa kuwafuatilia watoto wao wajishughulishe na kazi za msingi hususani wale wanaohitimu masomo, ambao alisema wanatakiwa kuangaliwa kwa karibu, ili wasijiingize katika makundi mabaya.

Pia aliwasihi wanafunzi wanaohitimu kutumia vizuri maarifa na ujuzi waliopata kujikwamua na hali ya maisha ya uraiani baada ya kutoka shuleni.

Mkurugenzi wa Shule hiyo, Peter Mutembei, aliwasisitiza wazazi na walezi kuwasimamia watoto wao katika nidhamu kama ambavyo wanadhibitiwa wakiwa masomoni.

Mutembei alisema shule hiyo inawafundisha watoto maadili mema na kusoma kwa bidii, ili kufaulu kwa wingi katika shule za vipaji maalumu.

"Kwa sasa tutaendelea na maboresho kuwa na darasa la kujifunza kwa kusoma na kuona, ili kuwaandaa katika mitihani yao ya ndani na ya kitaifa," alisema Peter.

Mkuu wa shule hiyo, Josia Philipo, alisema, moja ya mikakati ya shule hiyo ni pamoja na kuboresha taaluma, mazingira wezeshi yatakayowafanya wanafunzi kujifunza na kuelewa kwa urahisi.

Aliongeza kuwa wataendelea kushirikiana na wazazi na walezi katika malezi ya watoto, ili kuwajengea mazingira wale wanaohitimu waendelee kuwa na maadili mazuri.

# Wachimbaji wadogo, wajasiriamali wanolewa

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAJASIRIAMALI na wachimbaji wadogo wa madini mkoani Geita wameanza mafunzo maalumu yanayolenga kuwajengea uwezo wa kuendesha biashara zao kwa ufanisi na kwa viwango shindani vya kimataifa.

Mafunzo hayo ya siku tatu ambayo yanaratibiwa na kuendeshwa na benki hiyo na wadau, yalizinduliwa jana mkoani Geita na Mkuu wa Mkoa huo, Mhandisi Robert Gabriel, kwenye maonyesho ya dhahabu na teknolojia yanayofanyika mkoani humo.

Mhandisi Gabriel alitoa wito kwa wafanyabiashara na wachimbaji wadogo mkoani humo kuzingatia kanuni za utunzaji wa fedha na heshima ya matumizi ili kulinda na kukuza mitaji yao.

"Ninaomba sana wajasiriamali na wachimbaji wadogo kupitia mafunzo haya muweze kubadilika na mtoke kwenye mfumo wa kufanya shughuli zenu kwa mazoea na badala yake muhamie kwenye mfumo wa kisasa unaoheshimu ushauri wa wataalamu wakiwamo hawa wanaotoka kwenye taasisi za fedha kama benki ya NBC na taasisi na mamlaka nyingine zinazosimamia biashara nchini," alisema.

Alisema iwapo wadau hao watatumia vizuri rasilimali madini hususani dhahabu, ni rahisi kwao kufanikiwa huku akitolea mfano mabadiliko ya kisera na kiutendaji yalivyoongeza mapato yanayopatikana kutokana na madini katika mkoa huo.

Alitaja baadhi ya mada muhimu kwenye mafunzo hayo ni taratibu bora za uchimbaji madini, umuhimu wa ulipaji kodi na taratibu za kufuata, matumizi sahihi ya taasisi za kifedha na upatikanaji wa mitaji, umuhimu wa kuwa wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii na matumizi sahihi ya kemikali katika shughuli za uchimbaji madini.

"Mwisho wa mafunzo haya tunaamini walengwa watapata kufahamu namna bora ya kuweka mipango na mikakati ya kukuza biashara zao, namna ya kutafuta masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi, mambo yanayoangaliwa na benki kabla ya kumpa mfanyabiashara mkopo, sababu zinazosababisha biashara nyingi zife na tabia za muhimu kwa mfanyabiashara," alisema.

Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki kutoka Benki ya NBC, Jonathan Bitababaje, alisema pamoja na kuzitambulisha fursa za huduma na bidhaa za kibenki ikiwamo huduma ya Klabu ya Biashara, 'internet banking' na mikopo isiyo na dhamana kutoka benki hiyo, mafunzo hayo pia yatawasaidia walengwa hao kuzitambulisha fursa za kibiashara ambazo wajasiriamali na wachimbaji wadogo hususani wa mkoa wa Geita na mikoa ya jirani wanaweza kunufaika nazo.

"Benki ya NBC tumekuja na mkakati huu mahsusi wa mafunzo kwa wafanyabiashara kutokana na matokeo ya utafiti wa kitaalamu unaoonyesha kuwa takribani zaidi ya asilimia 70 ya biashara zote zinazoanzishwa hufa na kupotea kabisa ndani ya mwaka mmoja, na hili linatokana na sababu kadhaa ikiwamo kukosekana kwa mbinu za uongozi mzuri wa biashara," alieleza.

Alitaja sababu nyingine zinazoathiri biashara za wajasiriamali hao ni kukosekana kwa utaalamu wa muhimu katika maeneo muhimu ya biashara na kukosekana kwa uelewa mzuri wa mambo ya kifedha katika kuziendesha biashara.

Nao baadhi ya washiriki, walisema mafunzo hayo yatawasaidia kuwajengea uwezo wa kuziendesha biashara zao kwa ufanisi na kwa faida.

"Kupitia mafunzo haya tunatarajia kunufaika na katika maeneo tofauti yakiwamo kujua namna ya kutunza kumbukumbu za biashara, ubora wa bidhaa na huduma kwa wateja, uongozi wa kibiashara na namna ya kutangaza biashara zetu," alisema mmoja wa wajasiriamali hao, Neema Matta.

Mbali na Benki ya NBC mafunzo hayo yanaendeshwa na wataalamu kutoka TANTRADE, Tume ya Madini, TRA, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, GST, SIDO, NEMC, TBS, OSHA, NEEC na taasisi nyingine za kifedha.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati (mwenye suti ya drafti), akiangalia moja ya bidhaa za nyuzi zinazozalishwa na kiwanda cha nyuzi mkoani humo, wakati wa ziara yake jana ya kukagua shughuli za kiwanda hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wasimulia miezi miwili machungu ya corona

**Na Christina Mwakangale**

WASHIRIKI wa semina ngazi ya jamii, wamesema kipindi cha kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19 kuanzia Machi hadi Mei mwaka huu, kilikwamisha harakati za wanawake kiuchumi na kisiasa.

Mshiriki wa semina hizo mkazi wa Manzese jijini Dar es Salaam, Kennedy Machery, alisema harakati za mwanamke katika kujiandaa na mwaka wa uchaguzi 2020, unaweza kuleta matokeo ya ushiriki mdogo katika siasa.

Alisema pamoja na athari hizo, zipo changamoto walizokumbana nazo wanawake na wasichana kwa kukumbana na ukatili wa kijinsia.

"Mwaka wa uchaguzi kama miaka mingine, ni kawaida maandalizi ya ndani kwa ndani ya taasisi kuandaa kundi maalumu la wanawake wagombea namna ya kujipanga kukabiliana na ushindani katika siasa, ili wajiamini na kutoa hamasa kwa viongozi wanawake watarajiwa," alisema Machery.

Alibainisha kwamba athari za maandalizi duni kwa kundi hilo kunaweza kurudisha nyuma azma ya wanasiasa, wanawake wanaoibukia.

Pia, alisema kipindi hicho baadhi ya wanawake, familia zao zilikumbwa na changamoto za kiuchumi na kusababisha baadhi ya wanawake wanaoendesha familia zao, kusambaratika.

Mwezeshaji wa semina iliyofanyika wiki hii, Agness Lukanga ambayo iliandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), alisema ipo haja ya kuongeza hamasa ya wanawake kuendelea kuinuka kiuchumi na kujenga mazoea ya kukabiliana na changamoto zozote.

"Corona ilidumaza watu biashara zao hasa wanawake, kwa nchi za Afrika, hivyo inatakiwa kutambua namna ya kujiandaa kisaikolojia na namna ya kujipanga iwapo itatokea majanga kama ya hayo duniani," alisema Lukanga.

Mshiriki wa semina hizo kutoka Mabibo, Aloyce Anthony, alisema utamaduni wa kufuata kanuni za kiafya ikiwamo kunawa mikono iwe ni utaratibu wa kudumu.

"Kipindi cha corona ilionyesha namna watu wanavyoweza kuheshimu kanuni na taratibu, ilikuwa kila biashara, nyumba na maeneo ya taasisi za umma na binafsi unakuta utaratibu wa kunawa kabla ya kupatiwa huduma, hii ilipunguza magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu," alisema Anthony.

# Majaliwa: Serikali inawathamini wafugaji

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali inawathamini wafugaji na itaendelea kuboresha sekta yao.

Aliyasema hayo juzi wakati akiwasalimia wananchi waliojitokeza kumlaki kwenye kata ya Bukundi, Tarafa ya Nyaranje, wilayani Meatu, akiwa njiani kutoka Mkalama, Singida.


"Tunatambua na kuwathamini sana wafugaji kwa sababu tunajua mifugo ni fedha," alisema wakati akimwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, mgombea ubunge wa Jimbo la Meatu, Leah Komanya na mgombea udiwani wa kata ya Bukundi, James Sombi.

"Serikali yenu imedhamiria kuboresha sekta ya mifugo nchi nzima na ndiyo maana waziri mwenye dhamana ya mifugo, amekuwa anakutana na wafugaji nchi nzima, ili waeleze ni maeneo gani yanawapa kero."]

Alisema, serikali iliruhusu vijiji 920 kati ya 970 vilivyokuwa kwenye maeneo ya hifadhi virasimishwe, ili wananchi waendelee na ufugaji na kilimo.

Alisema, eneo la Bukundi lina wakazi wengi ambao asilimia 60 kati ya hao ni wafugaji. Amewaomba wagombea hao wakipita, warudi kwa wananchi na kutatua kero zao kwenye sekta ya mifugo.

Mapema, mgombea ubunge wa Jimbo la Kisesa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema wakati serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani, majosho 1,000 kati ya 2,400 yaliyokuwapo yalikuwa ni mabovu. "Chini ya uongozi wa rais wetu jemedari, Dk. Magufuli, majosho 600 yamekarabatiwa na tumejenga majosho mengine mapya 104. Yote yamepewa dawa ya ruzuku na wafugaji wanayatumia kuosha mifugo yao," alisema.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (kushoto), akimkabidhi Mganga Mkuu (RMO) wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Best Magoma, mashuka 180 kwa ajili ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma hivi karibuni. NMB walikabidhi msaada wa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 11. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yataka vijana kushiriki maendeleo

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kimesema kuwa vijana, makada na wanachama wa chama hicho wanayo nafasi kubwa ya kushiriki katika shughuli za maendeleo ikiwamo ujenzi wa miundombinu.

Kauli hiyo ilitolewa jana wilayani hapa na Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Kahama, Thomas Myonga, wakati akizungumza na wanachama kwenye ufunguzi wa ofisi mpya kata ya Kilago, Halmashauri ya mji wa Kahama, iliyojengwa kwa ufadhili wa vijana na wanachama wa CCM.

Alisema kuwa katika kukijenga chama, kundi la vijana ndani ni msingi imara wa maendeleo hivyo ni vyema wakawa wanakumbuka kuchangia na kukisaidia.

Aliwataka wananchi hasa vijana na kujitokeza kwa wingi kukipigia kura chama hicho ili kiweze kuendelea kushika dola na kwamba vijana wasishawishike kushiriki katika vurugu za kiasa badala yake washiriki kuhamasisha amani wakati wa uchaguzi.

Naye Godfrey Ihema, ambaye amefadhili ujenzi huo alisema, wataendelea kutumika na kusaidia CCM katika nafasi ya udiwani, ubunge, urais na kwamba chama kiendelee kuwatumia vijana katika jambo lolote la kichama na hata kiserikali.

## JKCI, taasisi ya Israel sasa kutibu moyo kimtandao

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na Kituo cha Matibabu cha Wolfson nchini Israel, wanaanzisha mifumo mipya ya kutumia teknolojia kutoa matibabu ya moyo kwa njia ya mtandao.

Kwa kutumia mfumo huo, madaktari bingwa wa nchi hizo mbili watashirikiana kwa njia ya mtandao kwa kutumia nyaraka za usalama wa data kufanya upasuaji kwa wagonjwa wa moyo wakiwa katika nchi zao.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Kituo cha Matibabu cha Wolfson, Dk. Lior Sasson, akizungumza kupitia taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, alisema kuanzishwa kwa mifumo hiyo kutaisaidia JKCI.

Alisema mfumo huo umeandaliwa kwa kushirikiana na timu ya Microsoft ili kuweka uwezo wa kiusalama na kutoa mwongozo kitaalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"Utekelezaji wa mifumo hii mipya itasaidia kutoa utambuzi sahihi na kupunguza idadi ya watoto wanaohitaji kusafiri kwenda Israel kupatiwa matibabu. Kwa upande wa kijamii, pia kuna faida zaidi kwa watoto wa JKCI, ambao wataweza kufurahia maisha," alisema Dk. Sasson.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Profesa Mohamed Janabi, alisema wataalamu wa upasuaji wanawasiliana mara kwa mara na wenzao wa Israel kupata ushauri.

"Tunafurahi kuwa ushirikiano huu na SACH na Microsoft utawezesha utambuzi sahihi kwa kutumia zana mbalimbali za kidigitali na kuleta manufaa kwa watoto walio chini yetu. Tunaingia kwa ujasiri katika ushirikiano huu wa matibabu na tunatarajia kuwa mstari wa mbele kufanikisha ubunifu huu," alisema Profesa Janabi.

Naye Kiongozi wa Maendeleo ya Biashara wa Microsoft 4 Afrika, Hustavo Raiter, alisema kama Microsoft wamepata faraja kuona ushirikiano ulianzishwa na taasisi hizo katika kuhakikisha wanaokoa maisha ya watoto nchini.

"Tunafuraha kuwa sehemu ya safari ya mabadiliko, ni fursa ya kweli na tuna hakika kuwa juhudi zao zitatumika kama mfano katika nchi nyingine," alisema Raiter.

# Babu Tale apewa kibarua barabara

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Morogoro, Hamdu Shaka, amemtaka mbunge mteule wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Hamisi Taletale (Babu tale) kusimamia na kutekeleza kipaumbele cha ujenzi wa barabara ya Bigwa Kisaki kwa kiwango cha lami, ili kusaidia wakulima wa maeneo hayo kunufaika na kilimo chao.

Alisema hayo jana, wakati akizindua kampeni katika jimbo hilo kuwa pamoja na kuwapo kwa vipaumbele vingi katika Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025, kiu kubwa ya wananchi wa jimbo hilo ni kupata barabara ya lami.

Alisema kuwa barabara hiyo yenye urefu wa zaidi ya kilometa 160 ndio chachu ya maendeleo katika Wilaya ya Morogoro kwa kutegemewa na wakulima kusafirisha mazao yao.

"Hapa tunazindua kampeni za kumwombea kura Dk. John Magufuli baada ya mgombea ubunge Babu Tale, kutangazwa kupita bila kupigwa, lakini tunamtaka atakapoapishwa kipaumbele cha kwanza kiwe hii barabara ya Bigwa Kisaki, ijengwe kwa lami kama ilani yetu ya CCM inavyosema," alisema Shaka.

Kwa upande wake Taletake, aliwaahidi kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Ilani ya CCM, ili kuwaletea wananchi maendeleo ikiwamo barabara hiyo ambayo imetajwa kuwa kero ya muda mrefu.

Alisema wakati anasubiri kuapishwa, ili kutekeleza ahadi zake, wananchi wamchague mgombea urais wa CCM, ili suala la kuleta maendeleo jimboni hapo litekelezeke kwa weledi mkubwa kwa kuwa chama hicho, ndio pekee chenye kujali watu wa hali zote.

"Nawaahidi wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki kuwa, baada ya kuapishwa kipaumbele changu cha kwanza, cha pili na cha tatu ni kujenga barabara hii ya Bigwa Kisaki, kwasababu najua wana Morogoro shughuli zetu kuu za kiuchumi ni kilimo, lakini ili kufanikisha haya nawaomba Oktoba 28, mwaka huu tumchague tena Rais Magufuli," alisema.

Alisema, anatambua kuwapo kwa changamoto ya huduma za afya katika baadhi ya vijiji na kata hasa ya upasuaji kwa wajawazito, hivyo atakapoapishwa atahakikisha vituo vyote vya afya vinakuwa na huduma hiyo.

# Hasunga avutiwa mpango mbolea bure

**Na Mwandishi Wetu,**
SONGWE

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amewataka wakulima wadogo nchini kujisajili katika mpango wa wakulima kupatiwa mbolea bure, ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao.

Akizungumza katika uzinduzi wa mpango huo , unaotekelezwa na Kampuni ya mbolea ya YARA Tanzania

mkoani Songwe juzi, Waziri Hasunga mbali ya kuvutiwa na kuipongeza kampuni hiyo kwa mpango huo,

aliwahimiza wakulima kuchangamkia fursa hiyo mapema.

"Nimevutiwa na mpango huu mzuri, ambapo mkulima anajisajili," alieleza na kuwataka wakulima kujitokeza kwa

wingi, ili waweze kunufaika na mpango huo unaolenga kuongeza uzalishaji wa mahindi na mpunga miongoni mwa wakulima wadogo. Waziri alisema kuwa mpango huo unaojulikana kama 'Action Africa' ni ubunifu wa hali ya juu na ambao utaleta mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa wakulima na kuchangia maendeleo ya viwanda nchini.

"Programu hii ya 'Action Africa' itasaidia sana kuongeza tija ya uzalishaji na kufanya Mkoa wa Songwe uwe na uhakika wa chakula pamoja na kujiimarisha kiuchumi kwa wakazi wake," alisema Waziri Hasunga.

Aidha, Waziri Hasunga aliongeza kuwa mpango huo mbali ya kuleta uhakika wa chakula, pia utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuzalisha malighafi za viwanda hasa ukizingatia serikali ya awamu ya tano imejielekeza katika wa ujenzi wa viwanda.

"Mpango huu licha ya kuwahakikishia wana Songwe na Watanzania kwa ujumla chakula na fursa za kuongeza mapato yao, utachangia katika upatikanaji wa malighafi ambazo zitakuwa muhimu kwa viwanda vyetu, ambapo tangu kuingia kwa serikali ya Rais John Magufuli imekuwa ikihimiza uchumi wa viwanda," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali mstaafu Nicodemus Mwangela, alisema mpango huo umekuja katika wakati muafaka mkoani humo na utachochea uzalishaji na kuinua mapato ya serikali. "Mkoa wa Songwe umekuwa ukizalisha kwa kiasi kikubwa na msaada huu wa YARA kwa wakulima wetu utatuhakikishia zaidi usalama wa chakula na kuweza kuuza chakula nchi jirani, ambazo zimekuwa zikitegemea sana kutoka mkoani Songwe," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa YARA Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema mpango huo ni jitihada za kampuni mama kutoka Norway kuhakikisha nchi za Afrika ikiwamo Tanzania zinajitosheleza katika kuzalisha chakula.

"Mpango huu wa 'Action Africa' umeasisiwa na kampuni yetu mama iliyopo nchini Norway na tunatarajia kugawa mbolea za NPK tani 12,500 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 16.5, nchini Tanzania ikilenga zaidi kukuza uzalishaji wa mahindi na mpunga," alisema Odhiambo.



Wakazi wa Kata ya Nyasa Jimbo la Masasi Mjini wakimsikiliza mgombea ubunge wa jimbo hilo, kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Hamza Machuma, katika mkutano wa kampeni juzi. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Mgombea ajinasibu kujenga kituo cha afya

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MGOMBEA udiwani kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Maili Moja, Ramadhan Lutambi, amesema atashirikiana na wananchi, serikali na wadau wa maendeleo kujenga kituo cha afya.

Lutambi aliyasema hayo juzi mjini Kibaha akiwa katika mkutano wa kampeni uliofanyika Maili Moja.

Alisema kata hiyo haina kituo cha afya kutokana na kuwa jirani na hospitali na vituo vya afya, hivyo kuwafanya wananchi kupata huduma za afya katika kata ya Tumbi.

Licha ya kata hiyo kuwa mjini na huduma za afya kupatikana kwa urahisi, alisema bado kuna mitaa ya mbali wananchi hutumia Sh. 4,000 ili kufika kupata huduma za afya kwa kutumia usafiri wa pikipiki.

Aidha, alisema katika kipindi kilichopita ipo miradi ya maendeleo aliifanya kwa kushirikiana na serikali, hivyo anaomba wananchi kumchagua kwa mara nyingine akamilishe yale aliyoyaanza.

Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Pwani, Musa Gama, alisema mwaka huu wamejipanga vizuri kwa kuweka wagombea ambao wanakubalika na wananchi.

Gama alisema hana wasiwasi na wagombea wao ambao wamejitolea kuwasaidia wananchi, ili kuwaondolea changamoto mbalimbali ili kuweza kuyafikia maendeleo, amewaomba wananchi kuwapa ridhaa wagombea wa CCM kuongoza kwenye kata, majimbo na nafasi ya Rais.



Ukurasa 14

## UTT mwokozi kipindi cha ukata

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 18, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

## Mkoa waanza maonyesho kuanika 'utukufu' wa madini



Muttamwega Mgaywa (mwenye suti) akisalimiana na baadhi ya wakazi wa Uwanja wa Fisi. PICHA: SABATO KASIKA

# Kampeni za uchaguzi zautaja uwekezaji wa Uwanja wa Fisi

**Na Sabato Kasika**

NI nadra kuwasikia wanasiasa wakiahidi kuwajengea makazi au kubadilisha nyumba duni za wapigakura nyakati za kampeni, lakini safari hii Chama cha Sauti ya Umma (SAU), kinaahidi kuwaletea maisha mapya wanaoishi eneo duni la Uwanja wa Fisi liliko Manzese Dar es Salaam.

Katika kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, mgombea urais wa SAU, Muttamwega Mgaywa, anatua katika eneo hilo na kutoa ahadi ya kuboresha mazingira na maisha kwa kuporomosha ghorofa na kujenga mji mpya wa Uwanja wa Fisi.

Akiwa katika kampeni Uwanja wa Fisi juzi, anasema, akichaguliwa ataubadili kwa kujenga ghorofa kama zilivyo za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ili wakazi wake waondokane na makazi duni.

"Niseme tu kwamba, nikichaguliwa kuwa rais, nitaanzia Manzese na hasa eneo hili la Uwanja wa Fisi, kwa sababu mazingira yake siyo mazuri na yanatakiwa kubadilishwa haraka iwezekanavyo," anasema Mgaywa.

Mgaywa anasema, yapo mengi ambayo chama chake kimeahidi kupitia katika ilani, miongoni mwake ikiwa ni kuboresha maisha ya Watanzania wakiwamo wa Uwanja wa Fisi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Muungano uliopo Uwanja wa Fisi, Joseph Mkude, anasema, kunahitajika uwekezaji mpya na kuboresha maisha.

Anatamani siku moja eneo hilo libadilishwe ili wakazi wake waondoke na uduni wa wa maisha na changamoto zilizopo sasa.

Mkude anasema, ingawa serikali inafanya juhudi mbalimbali kukomesha ukahaba bado upo, hivyo ni bora likabadilishwa na kuwekwa viwanda vidogo ili watu wapate ajira.

"Ni hatari watu kuishi kwa kutegemea kuuza miili yao, badala yake wanatakiwa kufanya kazi halali ya kuwaingizia kipato, ndiyo maana ninashauri Uwanja wa Fisi ubadilishwe na kujengwa viwanda vidogo ili waajiriwe,"anasema Mkude.

Kinachotakiwa ni kutafuta wawekezaji katika eneo hilo na kisha tathmini na malipo ya fidia yafanyike kupisha uwekezaji ili eneo hilo litumike kwa shughuli za maendeleo.

"Hatua hiyo italifanya eneo hilo kuheshimika, kuliko ilivyo sasa, wakazi wake wanadharaulika, kwa sababu wanaishi eneo ambalo lina sifa chafu zisizostahili katika jamii," anasema.

Mkazi wa eneo hilo, Betty Joshua, anasema, wanasiasa wanaotoa ahadi za kubadili Uwanja wa Fisi wanatakiwa kuzitimiza kuliko kupiga domo na kuacha hali ilivyo kwa miaka mingi.

### HALI ILIVYO UWANJANI

Kama yalivyo majiji mengine mengi duniani mfumo wa makazi unakaakisi hali ya kipato. Vivyo hivyo kwa Dar nayo imegawanyika katika makundi tofauti ya wakazi wakiwamo wenye kipato kikubwa, walio na uwezo wa kati na walalahoi.

Uwanja wa Fisi ni eneo ambalo linasifika kwa wakazi wake wengi kuishi maisha ya hali ya chini ya kutegemea vyakula vinavyouzwa kwa bei rahisi zikiwamo supu ya ngozi za wanyama.

Asilimia kubwa ya wakazi wa 'Uwanja wa Fisi', wana kipato cha chini, wanaishi katika lindi la umaskini kwa kushindwa kumudu gharama za maisha ikiwamo kupata chakula, dawa na mkazi.

Hali hiyo inawalazimisha kununua vyakula vya bei nafuu na wakati mwingine kutumia bidhaa ambazo muda wake wa matumizi umemalizika, kutokana na unafuu ama kutoelewa athari zake kiafya.

Ukifika katika maduka ya eneo hilo wafanyabiashara wanauza bidhaa kulingana na hali halisi ya maisha ya wakazi wenyewe, ili kuhakikisha kila mmoja anapata mahitaji yake ya kila siku.

Kwa mfano, katika maduka ya Uwanja wa Fisi, utakuta sukari, chumvi, majani ya chai na vitu vingine vinapimwa na kufungashwa katika vipimo vidogo ili kuuzwa kwa bei inayolingana na mahitaji ya kila mteja kwa kiwango ambacho anaweza kukimudu.

Aidha, mafuta ya kula nayo yana vipimo vidogo, lengo nikiwa ni kumfikia kila mlaji wa eneo hilo na kumpa mahitaji yake ya kila siku kulingana na uwezo kiuchumi.

Mwenye uwezo wa kupima sukari kwenye mizani atafanyiwa hivyo, anayetaka kununua ile ambayo imeshafungashwa katika vipimo vidogo atapata, ili mradi asiwepo mtu atakayekosa huduma.

### AHADI YA MABADILIKO

Kumekuwapo ahadi mbalimbali za kubadili mazingira na maisha ya Uwanja wa Fisi kuwa bora zikilenga kukomesha shughuli zote za kihalifu kama biashara ya ngono kwa watoto, vilevi haramu na mihadarati hata hivyo hazijatimia.

Miongoni mwa ahadi hizo ni ile ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, anapotembelea Uwanja wa Fisi na kuahidi nyumba zote za eneo hilo zitabomolewa na kujengwa viwanda.

Novemba mwaka 2016 anatoa ahadi hiyo na kusema, nyumba zote za eneo hilo zitabomolewa na kuwapa watu waendeshe viwanda vidogo vidogo, lakini kwanza ifanyike tathmini ili wenye nyumba walipwe haki yao.

"Nimejionea hali ilivyo katika maeneo ya Mtaa wa Fisi si mazuri, nitatafuta wafanyabiashara wa viwanda vidogo wanunue eneo hili...," anasema Makonda.

Anasema nia ni kupata Dar es Salaam mpya kuliko ilivyo sasa kwenye eneo hilo: "Mara baada kufanya ukaguzi nikajiridhisha na hili ndilo tamko langu kwa umma kwa wananchi wa mkoa huu," anasema, hata hivyo, ameondoka kabla hajatimiza ahadi yake.

BIASHARA

# Mkoa waanza maonyesho kuanika 'utukufu' wa madini

• Kuvuta wageni kitaifa, kimataifa



Wachimbaji wadogo wa dhahabu wakiwa kazini mkoani Geita.

**Na James Lanka**

LEO ni leo mkoani Geita, ile siku iliyokuwa inatarajiwa na wachimbaji madini na wawekezaji kwenye sekta hiyo imewadia.

Ni maonyesho ya teknolojia na uwekezaji kwenye sekta ya dhahabu yanayoanza wiki hii Septemba 17 yakitarajiwa kuendelea hadi Septemba 27.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, anasema maonyesho kama hayo mwaka jana yalifanyika katika eneo la ekari saba kwenye viwanja vya CCM Kalangalala lakini mwaka huu yameboreshwa zaidi na kutakuwa na mambo mengi ya kuvutia hasa katika sekta ya madini na kuwaomba wananchi na wawekezaji kujitokeza kuwania fursa zitokanazo na maonyesho hayo.

"Tumeshatengeneza eneo la ekari 15 kwa ajili ya maonyesho ya teknolojia na uwekezaji ya madini mwaka huu. Ninatoa wito kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki katika maonyesho hayo ya kimataifa," anasisitiza Gabriel.

Anaendelea kufafanua kuwa maonyesho hayo makubwa ya kimataifa anaamini yatavutia watu kutoka mataifa mbalimbali ambayo yataonyesha bidhaa mbalimbali, pia kutakuwa na ushiriki wa taasisi mbalimbali nyeti za fedha kama benki, taasisi zote za madini, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), mitambo mbalimbali ya kuongeza thamani madini na hata kwenye mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

"Natoa wito kwa wajasiriamali kujitokeza kwa wingi ili waje wakutane na teknolojia pamoja na wataalmu mbalimbali wa uchimbaji, watoa mikopo, uwezeshaji katika sekta hiyo ya madini na hata kilimo, ufugaji na uvuvi," anasisitiza Gabriel.

Aidha, anasema mkoa unajenga jengo jipya litakalojulikana kama Geita Mining Complex lililopo katika hatua ya mwisho ya ukamilikaji.

Anausifu mkoa huo kuwa ni miongoni mwa mikoa yenye fursa nyingi za uwekezaji, hasa katika sekta ya madini ya dhahabu na kwamba ni eneo nyeti la kuanzishwa migodi na viwanda vya kuchakata madini.

Anasema hazina ya madini inayopatikana Geita ni kubwa kuliko ya sehemu nyingine zote nchini tena dhahabu inachimbwa katika wilaya zote tano za mkoa huo za Geita, Nyang'hwale, Mbogwe, Ushirombo na Chato.

Anaeleza kuwa mgodi mkubwa wenye dhahabu nyingi ni Geita Gold Mine (GGM), unaozalisha dhahabu kwa wingi kwa wakati mmoja kuliko mingine yote mikubwa nchini.


Akizungumza na Nipashe anasema shabaha ya mkoa ni kuvuta wawekezaji wa viwanda na biashara ili kuongeza kasi ya kukuza uchumi na kuchangia kukuza pato la taifa.

Ili kutimiza azma mkoa umeandaa eneo maalumu lenye ukubwa wa ekari 300 kwa ajili ya uwekezaji kibiashara na utalii.

Akizungumzia hatua ya ujenzi wa eneo jipya la uwanja wa maonyesho ya biashara, Mkuu wa Mkoa wa Geita, wakati alipotembelea eneo la ujenzi anasema lengo kubwa ni kuendeleza maonyesho ya teknolojia ya kuchimba dhahabu, ambayo kwa mara tatu mfululizo yamefanyika mkoani Geita.

Mkuu huyo wa mkoa anafafanua kuwa, jengo hilo jipya litakalojulina kama Geita Mining Complex lipo katika hatua ya mwisho ya za kuelekea kukamilika na kuwaahidi wananchi wategemee jengo hilo la kisasa litakuwa sehemu muhimu ya biashara ya dhahabu. Anasema jengo lipo kwenye eneo la ukubwa wa hekari 100 kati ya 300 zilizotengwa na serikali.

> **Mkoa unajenga jengo jipya litakalojulikana kama Geita Mining Complex lililopo katika hatua ya mwisho ya ukamilikaji.**



Maduka ya sonara kuchonga vito na kuuza bidhaa za dhahabu ni miongoni mwa uwekezaji mkubwa unaotarajiwa kufanyika mkoani Geita. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### FURSA KIBAO

" Mkoa wetu tunazo fursa nyingi za kiuchumi ikiwamo uwanja wetu wa ndege wa Chato, hifadhi ya taifa ya kisiwa cha Rubondo na Chato-Burigi hivyo ni vyema tukaanza kuchangamkia uwekezaji huo kwa kuwekeza kwenye hoteli zenye hadhi, ili watalii wanaokuja kutembelea hifadhi zetu wapate huduma hizo,"anafafanua Gabriel.

Anasema anaamini siku za usoni Geita utakuwa mkoa wenye uchumi mkubwa wa madini ya aina mbalimbali hasa dhahabu na utalii akiwaomba wawekezaji mbalimbali kujitokeza kuzichangamkia fursa hizo adimu za kiuchumi.

### UJENZI WA VIWANDA

Mkuu wa Mkoa anaongeza kuwa aidha, zimetengwa hekari 200 kwa ajili ya uwekezaji na kwamba vitajengwa viwanda vya kutengeneza juisi za matunda ya aina mbalimbali, viwanda vya kuzalisha maji ya kunywa, maduka ya sonara wanaouza hereni, mikufu, pete, pamoja na hoteli za kitalii za hadhi ya nyota tano, huku hekari 100 ni kwa ajili ya viwanda vidogo.

Mhandisi wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Meja Samuel Hagu, akizungumzia ujenzi wa jingo Geita Mining Complex, anasema kazi iko kwenye kujenga jengo la utawala inayofanyika kuanzia Februari mwaka huu na kwa sasa umefikia asilimia 95.

Kwa upande wa uwanja wa maonyesho yanayoanza wiki hii anasema umefikia asilimia 75 na kwamba kazi kubwa iliyobakia ni upakaji wa rangi na katika upande wa uwanja tayari kazi imefikia asilimia 75.

Leonard Bugomola ni mmoja wa wadau wa madini Geita, ambaye pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri anafafanua kuwa, kutokana na kutambua umuhimu wa ujenzi wa jengo hilo ili kukuza sekta ya madini mkoani Geita, halmashauri hiyo ilikubaliana kupunguza matumizi ya fedha za ziara na kuzielekeza katika ukarabati wa eneo la maonyesho hayo muhimu ya madini.

"Nitumie nafasi hii kuishukuru sana kampuni ya GGML wadhamini wetu wakubwa wa maendeleo kwani wametusaidia kwa kipindi chote kuhakikisha maeneo yote ya uwanja wa maonyesho yanakuwa safi."

Kwa upande wake Msimamizi Mkuu wa Miradi ya ujirani mwema (CSR) wa GGML, Moses Lusasa, anafafanua kuwa kampuni imegharamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za afya, elimu, miundombinu na maji.

"Kupitia miradi yetu ya CSR, tumekuwa tukipanda Mlima Kilimanjaro kila mwaka kuchangisha fedha za kukabiliana na athari za VVU na Ukimwi ikiwa ni sehemu ya kuisaidia serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo,' anasema Lusasa.


Mkoa wa Geita upo Kanda ya Ziwa una dhahabu inayoufanya kuwa eneo muhimu katika kuvutia uwekezaji na maendeleo ya biashara za ndani na za kimataifa.

Aidha, umezungukwa na Ziwa Victoria lenye samaki wenye ladha ya kipekee na murua jana sato na sangara.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Bosi ukipewa dhamana jiamini






**NA JOSEPH KULANGWA**

KUNA mama ambaye alikuwa akiishi na mwanawe mchanga, huku akifuga mbwa, ambaye alikuwa mtiifu sana kwake na kila alipoondoka nyumbani kwenda kutafuta mahitaji, alimwacha pembeni mwa kibanda kidogo cha mwanawe akimlinda.

Kwa kweli mbwa huyo aliifanya kazi yake ya ulinzi vizuri na hata mtoto alipokuwa akimwona pembeni akiwa lindo, alitulia utadhani hayupo, hakulia mpaka mama yake aliporudi na kumpa mahitaji yake na kuendelea kulala kama si kuchezea wanasesere.

Mama huyo alijenga imani kubwa sana kwa mbwa yule na alimpa matunzo aliyostahili ya chakula, tiba na chochote ambacho mbwa alitakiwa kukipata, ikiwa ni kuonyesha shukrani yake kwa kumsaidia malezi ya mwanawe huyo.

Siku moja mama kama kawaida yake, aliondoka kwenda sokoni na kumwacha mbwa akiwa lindo. Baada ya muda alirejea na mahitaji yake, lakini akashikwa butwa akukutana na matambara yaliyozagaa sakafuni na mengine yakiwa na damu.

Moyo ulimshituka na ghafla akakumbuka kwenda chumbani alikomwacha mwanawe kwa kasi kubwa, huku akiwa hajui nini kimetokea. Akakutana na michirizi ya damu na kitandani hamwoni mwanawe. Mara moja akili ikampa kuwa mbwa yule kamgeuka mwanawe na kumtafuna.

Mama akamwita yule mbwa kwa hasira, naye akajitokeza mbele yake akitikisa mkia kuonyesha utiifu, huku midomo ikiwa imetapakaa damu na nyingine ikiendelea kudondoka kutoka kinywani. Mama mtoto akapandwa na hasira akijua tayari ni ushahidi kuwa mbwa amemtafuna mwanawe.

Bila kusita akakimbilia jikoni na kutoka na rungua kalitumia kumpiga yule mbwa mpaka akamuua pale pale,naye akaanza kulia kwa uchungu wa kupoteza vipenzi vyake kwa wakati mmoja. Kama vile mtu asiyeamini akarudi kuangalia kitanda cha mwanawe.

Alipokizunguka akamkuta mwanawe yuko chini amelala na anapumua kana kwamba hakuna lililotokea. Mama akashusha pumzi na alipoangalia chini akaona michirizi ya damu chini ya kitanda cha mtoto, na alipochungulia akaona joka lililouawa na kunyofolewa nyofolewa na kubaki na vidonda.

Safari hii akachanganyikiwa zaidi, hata akili zilipomrejea na kubaini kwamba kumbe alipoondoka joka liliingia ndani kwa lengo la kumdhuru mtoto na kama si ujasiri wa yule mbwa kupambana nalo na kuliua, mtoto asingekuwapo tena. Mama akalia sana, akijutia kwanza kwa kumwonea mbwa yule, pia kwa kumpoteza msaidizi wake muhimu.

Inatufunza nini hii? Si vema kuchukua hatua kabla ya kuridhishwa na jambo. Si vizuri kuhukumu tu kabla ya kupata uthibitisho wa tuhuma hizo. Haya yanatokea sana katika jamii zetu, yanatokea sana hata miongoni mwa viongozi wetu huku mitaani na kwingineko.

Kiongozi anaweza kusikia kwamba mahali anakokusimamia yeye kuna tatizo na bahati mbaya tatizo hilo limegundulika baada ya mkuu wake kupita eneohilo na kulalamika. Lakini, badala ya kujiridhisha, kiongozi anaamua kumwadhibu msimamizi wa eneo hilo, bila yeye mwenyewe kwenda eneo la tukio kushuhudia tatizo.

Wakati mwingine hutokea mhusika kubaini kuwa kakosea na kufuta adhabu, ambayo pengine mwathiriwa anakuwa ameanza kuitumikia na hivyo kumwathiri kisaikolojia, pia kuchafuka machoni mwa umma.

Mbwa yule asingeuawa, kama mama angejipa muda wa kuchunguza na kujua nini kilichojiri.

Hali hiyo mara nyingi huchangiwa na mtu kutojiamini au kufanya kazi wa nidhamu ya uoga, kwamba kama mkuu wangu kaona tatizo wakati mimi silijui, itakuwaje? Hivyo, anafikia hatua ya kutoa adhabu ya uonevu kwa sababu tu ya upungufu wake.

Uongozi ni kujiamini, kusimama penye msimamo wa usahihi na kusaidia hata kutafuta njia ya kurudi kwa mkuu wako kurekebisha, pale uhahisi kapotoka, maana naye ni binadamu, hajakamilika.

Pia, unapokuwa umepewa dhamana ya kusimamia jambo ni vizuri ukalisimamia na kulifuatilia kila mara, ili isijetokea likasimama na kujikuta unaumbuliwa na mkuu wako, ambaye pengine anakuwa amepita kwenye jambo hilo bila ya wewe kujua. Siku utembeapo mtupu, ndipo hukutanana mkweo. Madisii, maarasii, mawaziri mpo? Alamsiki!

Simu: (+255) 713 410008 na

BIASHARA

# UTT mwokozi kipindi cha ukata

• Hulipa ada, bima, ni akiba ya kujikimu kimaisha



Ofisa Masoko na Uhusiano UTT AMIS, Rahim Mwanga, akiwapa wadau taarifa mbalimbali: **PICHA UTT-AMIS**

**Na Frank Monyo**

ILI kufanikisha maendeleo ya watu na taifa kwa wakati mmoja mbinu nyingi hutumika kama kuwa na wanachama wanaowekeza kwa pamoja. Hapa nchini, jitihada hizo zinafanywa na kampuni ya Unit Trust of Tanzania-UTT AMIS iliyo chini ya Wizara ya Fedha.

Wiki iliyopita tuliangalia historia, majukumu na faida za uwekezaji huo unaohusisha wananchi (wanachama) wa aina mbalimbali na namna wanavyoweza kunufaika na mifuko ikiwamo ya Wekeza, Umoja na Mfuko wa Watoto, leo makala inaanza kwenye mfuko mwingine wa UTT-AMIS unampa faida

**MFUKO WA HATIFUNGANI**

Anapoanza kuzungumzia mfuko wa hati fungani Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Masoko na Mahusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga, anasema mfuko wa hatifungani au bond fund unatoa fursa kwa mwekezaji kufurahia faida shindani inayopatikana kwenye hatifungani mbalimbali za serikali kwa lengo la kukuza mtaji na kupata gawio aidha kwa utaratibu wa mwezi au nusu mwaka.

Kwa mpango wa kukuza mtaji kiwango cha chini huanza na kuwekeza Sh.50,000, kwa gawiwo la kila mwezi Sh. milioni 10 na Sh.5,000,000 kwa gawiwo la kila baada ya miezi sita.

"Tuna mifuko ya aina mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya wawekezaji na kuleta ushiriki mpana zaidi kwenye masoko ya fedha na mitaji,"anasema Mwanga.

> **"Katika kikundi chetu tuna michango ya wiki na ule mkubwa wa mwezi, fedha hizo zote tumekubaliana wanachama wote kutoa asilimia 10 kwa kila michango itakayopatikana na kuwekeza kupitia mfuko wa ukwasi.**

**MAFANIKIO KIUWEKEZAJI**

Mwanga anasema tangu kuanza Mfuko wa Umoja mwaka 2005 yapo mafanikio makubwa ikiwamo kuongezeka; mifuko na wawekezaji, rasilimali za mifuko, kutoa faida shindani kwa wawekezaji na kuaminiwa wawekezaji katika sekta ya masoko ya fedha na mitaji.

"Tulianza na mfuko mmoja sasa tunayo sita ya uwekezaji, lakini pia wakati mfuko unaanza 2005 tulikusanya zaidi ya Sh. bilioni 90 kutoka kwa Watanzania. Sasa hivi tunajivunia kufikia zaidi ya Sh. bilioni 420 ambazo tunazisimamia. Ni kilelezo kwamba wananchi wanatuamini na wanaona UTT AMIS ni sehemu salama ya kuwekeza fedha," anasema Mwanga

"Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa wawekezaji kutoka 80,000 mwaka 2005 hadi zaidi ya 160,000 mwaka 2020. Japo changamoto ni kuwafikia watu wengi zaidi," anaongeza kuwa .

UTT-AMIS imejitanua zaidi na kufika kwenye maeneo mengi wanakopatikana wawekezaji husussan mikoani.

"Tuna ofisi Arusha, Dodoma na Dar es Salaam pia mawakala wapo nchi nzima kupitia Matawi ya Benki ya CRDB ambapo wawekezaji wetu wanapata huduma. Hapo awali ilimbidi mwekezaji kufika benki kununua vipande, lakini leo anaweza kuvinunua kwa njia nyingi kama benki, simu na mitandaoni kwani teknolojia inaruhusu,"anasema Mwanga

Anaeleza kuwa mifuko imekuwa ikivuka vigezo vya ushindani mfano mfuko wa ukwasi kigezo cha kujilinganisha na soko ni hati fungani ya siku 35 ambapo faida yake ni asilimia mbili kwa mwaka lakini mfuko unatoa faida kati ya 12 hadi 14 kwa mwaka hivyo kuvuka matarajio ya wawekezaji.

**MAONI YA WANUFAIKA**

"Nilikuwa na ndoto ya kufanyabiashara ya kuagiza mabegi ya shule kutoka China lakini likaja tatizo la corona, mipaka ikafungwa na biashara zikasimama hasa China, kwa hiyo ile pesa niliyotaka kuagizia mzigo ikanibidi niwekeze katika katika Mfuko wa Ukwasi(liquid fund) huku nikisubiria hali ikae sawa," anasema Samson Nyamaka

Nyamaka ambaye ni mkazi wa Sinza Dar es Salaam anasema kuwa elimu ya kuweka akiba na kuwekeza aliyopewa na maofisa wa mfuko huo imempa mwanga katika safari yake ya kuwa mfanyabiashara mkubwa kwani pesa alizowekeza katika kampuni hiyo zinaongezeka na kukuza mtaji.

"Nilijiunga katika mfuko wa Kujikimu, ambao unatoa gawio mara kwa mara huku lengo kubwa likiwa kukuza mtaji kwa muwekezaji hivyo pesa niliyoweka zaidi ya 5,000,000 nategemea kupata gawio baada ya mwaka na nitakuwa nimeongeza mtaji wangu katika biashara niliyotamani kufanya," anasema Nyamaka

Mariam Mrosso, anayeishi Kurasini Dar es Salaam pia, anasema kuwa kampuni ya UTT AMIS imempunguzia mzigo wa ada ya mtoto wake baada ya kufiwa na mume mwaka 2009.

Baada ya kifo cha mume, mwaka uliofuata alifungua akaunti ya katika Mfuko wa Watoto, UTT AMIS kwa ajili ya ada ya kumsomesha sekondari na chuo kikuu.

"Mume wangu alivyofariki aliniachia mtoto mmoja akiwa na miaka mitatu, niliwaza sana juu ya maisha yangu na elimu ya mtoto kwa sababu nilikuwa ninafanya biashara ndogo ndogo stendi ya daladala Kurasini," anasema.

Mwaka 2010 akiwa kwenye Maonyesho ya Biashara ya Sabasaba alipita kwenye banda la UTT AMIS akapewa maelezo jinsi mifuko yao inavyofanya kazi akavutiwa na ule wa watoto na kujiunga.

Amesema baada ya kujiunga alikuwa akichangia Sh.20,000 kwa mwezi ndani ya miaka 10 mpaka sasa na kwamba kwa sasa mtoto wake yupo darasa la saba na mwakani anategemea kuingia sekondari hivyo hana wasiwasi na suala la ada ya mtoto wake. Mzee Sadiki Mshiyu, ambaye ni mstaafu katika taasisi moja ya kiserikali ambayo hakutaka kuitaja jina lake, amesema kuwa UTT AMIS imemsaidia kutunza fedha zake za kiinua mgongo kwa faida huku akifanya utafiti afanye biashara gani.

Anasema kuwa kati ya fedha zake za kiinua mgongo alizolipwa aliamua kuwekeza katika mfuko wa hati fungani una lengo la kutoa gawio kila mwezi na kila baada ya miezi sita huku piakukiwa na mpango wa kukuza mtaji.

"Nilipostaafu kazi nilifuatilia mafao yangu na nilipata tu, niliwatafuta UTT AMIS na kuwekeza milioni 50 ambayo kwa mwezi napokea wastani wa Sh 500,000 ambayo inanitosha kufanya shughuli zangu na kuendesha maisha," anasema.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Nyota Njema cha Dar e Salaam, Frida Lyatuu, anasema kikundi chao ni wawekezaji wa UTT AMIS kwa zaidi ya miaka mitatu.

Anaeleza kuwa wamepata manufaa makubwa kupitia uwekezaji kwa kufanya miradi mbalimbali ukiwamo wa ufugaji wa samaki.

"Katika kikundi chetu tuna michango ya wiki na ule mkubwa wa mwezi, fedha hizo zote tumekubaliana wanachama wote kutoa asilimia 10 kwa kila michango itakayopatikana na kuwekeza kupitia mfuko wa ukwasi," anasema.

Mwanga anasema mfuko wa ukwasi unawekeza katika dhamana zenye kutoa mapato ya kudumu. Hivyo muhimu na bora kwa wekezaji wanaotaka uhakika wa faida na kutunza mitaji yao.

Anaeleza kuwa hivi sasa kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza kwenye mfuko huo Sh.100,000 na kiwango cha chini cha nyongeza ni Sh.10,000.





# Wataalamu afya wapewa miezi sita leseni

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imeagiza wataalamu wa sekta ya afya nchini kusajili na kuhuisha leseni kwenye mabaraza yao ya kitaaluma ndani ya miezi sita kuanzia sasa.

Sambamba na hilo, imewataka waliojiendeleza kitaalamu kuwasilisha vyeti vyao vya viwango vya elimu katika mabaraza ili kutambulika kisheria na kitaaluma.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wasajili wa mabaraza mbalimbali ya kitaalamu ya Wizara ya Afya pamoja na wasajili wa bodi zilizo chini ya wizara hiyo.

Alibainisha kuwa kila mwanataaluma aliyemaliza mafunzo yake anatakiwa kujisajili katika mabaraza ya kitaaluma.

"Agizo hili ni kwa wanataaluma wote katika sekta ya afya, ili mtambulike na uzuri hivi sasa kuna tovuti hivyo mnaweza kupata kujisajili, kulipia na baadaye kutumiwa vyeti vyenu bila kuchelewa, kwa mantiki hiyo nawapa miezi sita wawe wamesajiliwa," alisisitiza.

Aidha, alisema kwa waliojiendeleza kwa ngazi mbalimbali ya taalauma ya afya kama shahada ya uzamili na uzamivu wanatakiwa kusajili viwango hivyo katika mabaraza yao ili watambulike.

Prof. Makubi alisema utaratibu huo umewekwa na serikali kupitia mabaraza hayo, hivyo kila mwana taaluma anatakiwa kujisajili au kuhuisha leseni ambazo zimeisha muda ili waendelee kutambulika na kufanya kazi zao. Kwa upande wa baadhi ya watu wa sekta ya afya wanaojipa hadhi ya kiwango fulani cha taaluma bila ya kujisajili kwenye mabaraza ya kitaaluma, Prof. Makubi alitoa miezi mitatu kwa wale wanataaluma wenye vyeti vyao wajisajilii ili kutambulika wapo katika kiwango fulani cha taaluma.

"Kuna baadhi ya wataaluma wanaojipa hadhi ya kiwango fulani cha kitaaluma wakati hawajasajili vyeti vyao kwenye mabaraza, nitoe mfano kuna wanataaluma wanaojiita mabingwa wa kitu fulani (specialist, consultant ...) na wanajitangaza kwa wananchi wakati hatuna ushahidi na kumbukumbu," alisema.

Alisema wamekubaliana na mabaraza suala hilo sasa lifike mwisho na wote waliojiendeleza zaidi wajisajili haraka kwa kuwasilisha vyeti vyao.

Kadhalika, aliwaagiza waganga wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa hospitali, taasisi za afya, vyuo vya afya na waganga wafawidhi wote kuzingatia kusimamia utekelezaji wa maagizo haya kwenye sekta zote za afya ili kulinda viwango na hadhi ya taaluma husika.

"Taaluma zote za afya lazima ziendelee kuheshimika na kusimamiwa vizuri ili kulinda afya za wananchi kwa viwango vya juu na bila kuruhusu wanataaluma bubu," alisema.

Aliwataka waganga wa tiba asili kufuata utaratibu wa kujisajili pamoja na wasaidizi wao na kufuata miongozo ya utoaji wa tiba asili na tiba mbadala kwa kuwa serikali ipo tayari kuwapa ushirikiano kwa kuwasaidia malengo yao ya utoaji wa tiba asili yanafanikiwa.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene (kushoto), akimkabidhi zawadi mwanafunzi Fabian Shija wa Shule ya St Charles ya mkoani Iringa baada ya kuongoza kwenye shindano la kitaifa la kuandika insha lililoandaliwa na ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu mazingira. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Hadhari kuwatibu kwa miti shamba watoto wenye kisukari

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

JAMII imetakiwa kuacha kuwapa watoto wao wenye ugonjwa wa kisukari dawa za mitishamba ambazo hazina vipimo na viwango.

Akizungumza na waandishi wa habari katika kambi maalum ya siku tatu kwa ajili ya watoto hao iliyoratibiwa na Chama cha Kisukari Tanzania, mmoja wa watoto wenye ugonjwa wa kisukari, Neema Paul, alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwapa watoto wao dawa hizo wakiamini zinatibu ugonjwa huo badala ya kuwahimiza kutumia dawa za hospitalini.

"Kuna baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwapa watoto wao dawa za miti shamba, hili si jambo jema, maana badala ya kupambana na tatizo moja, mtoto ataanza kuhangaika na magonjwa mengine kama figo na msongo wa mawazo," alisema.

Kadhalika, aliitaka jamii kuacha kuwanyanyapaa watoto wenye tatizo la kisukari na badala yake wanatakiwa kusaidia ili watimize ndoto zao.

Naye Moses Paul kutoka kliniki ya Bugando, aliwashukuru waandaaji wa kambi hiyo kwa kuwa amejifunza mambo mengi ambayo awali alishindwa kuyazingatia.

Alitolea mfano suala la mlo ambalo limesaidia kujua anatakiwa kula vyakula vya makundi gani. Alitumia fursa hiyo kumuomba Rais John Magufuli kusaidia upatikanaji kwa wingi kwa dawa za kisukari katika maeneo mengi.

"Popote pale Rais John Magufuli akinisikia, tunaomba kuongezewa kwa dawa za kisukari ili hata wale wanaotoka kwenye familia maskini wapate huduma hii hususani watoto," alisema.

Naye Mratibu wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA), Happy Nchimbi, alisema kambi hiyo inalenga kutoa elimu ya namna ya kuenenda na ugonjwa wa kisukari kwa watoto na wazazi.

Alisema watoto 28, wazazi na watoa huduma kutoka kwenye kliniki saba za Bugando na Seketure (Mwanza), Nyakaanga na Rubya (Kagera), Singida, Mbeya na Dodoma wamepatiwa mafunzo.

Aidha, alisema kambi nyingine ya Bagamoyo ilishirikisha washiriki kutoka mikoa ya Dar es Salaam yenye kliniki nne, Tanga, Kilimanjaro na Arusha.

"Jamii inapaswa kujua kuwa tatizo hili halimfanya mtoto kuwa wa tofauti, hivyo wanapaswa kusaidia kazi za nyumbani na kushiriki michezo, ili kulielimisha hilo, mbali na masomo tumekuwa tunawashirikisha katika shughuli mbalimbali, kila asubuhi tukiamka watoto wanakwenda kwenye mazoezi, kabla ya mazoezi tunawapima na ambao wako katika hali nzuri ya kushiriki mazoezi anashiriki," alisema.

Daktari wa watoto anayetoka Wizara ya Afya katika idara ya tiba kitengo cha magonjwa yasiyoambukiza, Dk. Julieth Kabengula, alikishukuru chama hicho kwa kusaidia ustawi wa watoto wenye kisukari.

Alisema tatizo hilo lipo na linakuwa kwa kasi na kubainisha kuwa katika kambi 38 ambazo Chama cha Kisukari Tanzania wanasaidia zimesajili watoto 4,000 wenye tatizo hilo.

# GePG ilivyoongeza makusanyo serikalini

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa kupitia mfumo wa kielektroniki (GePG), serikali imeongeza makusanyo ya kila mwezi na kupunguza gharama za uendeshaji.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, kupitia mfumo huo makusanyo ya mwezi yameongezeka kutoka Sh. bilioni 668 mwaka 2015/2016 hadi kufikia Sh. trilioni 2.6 mwezi juni, 2020.

Akiwasilisha juzi matokeo ya utafiti wa mfumo huo, Profesa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Joel Mtebe, alisema tathmini iliyofanywa kwenye mfumo huo ni katika ukusanyaji wa kodi, maduhuli, tozo na huduma mbalimbali.

Alisema mfumo huo umeongeza uwazi na udhibiti katika ukusanyaji wa fedha za umma na kupata taarifa sahihi na kwa wakati zinazohusu makusanyo.

"Kwa mfano Mamlaka ya Maji Kasuru walikuwa wanatumia kati ya Sh. milioni 1 hadi 1.5 kwa mwezi kusambaza ankra za maji kwa kutumia pikipiki, lakini imepungua kwa kiasi kikubwa ambapo kwa sasa wateja wanapata kupitia mfumo huu," alisema Prof. Mtebe.

Aidha, alisema Shirika la Umeme nchini(Tanesco), wameokoa Sh. bilioni 38 ambazo zilikuwa zinatumika kwa mwaka kuwalipa mawakala wa kuuza umeme.

"Pia Wakala wa Misitu (TFS) makusanyo yameongezeka kutoka Sh. bilioni 95 kwa mwaka hadi Sh. bilioni 115, Wakala wa Vipimo (WMA) mapato yameongezeka kutoka Sh. bilioni moja kwa mwezi hadi Sh. bilioni 2.5," alisema.

Alisema kupitia mfumo huo wananchi wanafanya malipo mahali popote bila kupoteza muda wa kwenda maofisini.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), William Erio, alisema mfumo huo umeongeza mapato ya shirika kutoka Sh. bilioni 694 mwaka 2018/19 hadi Sh. trilioni 1.1, Juni 2020.

Erio alisema mfumo huo umesaidia kuondoa malipo hewa yaliyokuwa yakifanyika kwa njia ya kuandika hundi bandia zilizokuwa zinalisababishia hasara shirika.

Kadhalika, alisema mfumo huo umefanikisha kuongeza thamani ya shirika kutoka Sh. trilioni 3.4 hadi kufikia Sh. trilioni 4.4 Juni 2020 na umepunguza gharama za uendeshaji kutoka akaunti 78 na kubaki tatu tu pamoja na kuweka uwazi kwa wateja wao na kupunguza miamala.

Akizungumza baada ya kupokea ripoti, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, aliwashukuru watafiti hao kwa kuandaa na kufanikisha utafiti huo ambao unaonyesha kuwa serikali imebuni mfumo sahihi wa ukusanyaji mapato.

James alisema serikali imebuni mifumo minne ya kielektroniki ambayo imetengenezwa na kusimamiwa na wizara hiyo hivyo ni salama kwa sababu inaendeshwa bila kuingiliwa na mtu wa nje.





# 'Mbegu bora hazitumiki kwa wingi Nyanda za Juu'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, umebaini kuwa kati ya asilimia 50 mpaka 70 ya wakulima wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini hawatumii mbegu bora hali ambayo inapunguza tija kwenye uzalishaji.

Watafiti wa kituo hicho waliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kuwawezesha wakulima hasa vijana kuzalisha mbegu bora wao wenyewe ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa mbegu hasa wakati wa mvua ambapo kila mkulima huwa anataka mbegu.

Mmoja wa watafiti hao, Fredrick Mlowe, alisema wananchi wa mikoa hiyo wana bidii kubwa kwenye kilimo, lakini tatizo ni kwenye matumizi ya mbegu bora na kwamba endapo wangekuwa wanatumia mbegu hizo wangekuwa wanapata tija zaidi.

Alisema wameamua kuanzisha mafunzo hayo ili kuwawezesha wakulima kuzalisha mbegu bora kwenye mazingira yao wenyewe badala ya kusubiri zizalishwe na vituo vya uzalishaji wa mbegu kwa maelezo kuwa wakati mwingine huwa vinazidiwa.

"Tunadhani kuwa wakizalisha wenyewe itakuwa rahisi hata bei ya mbegu kushuka na hivyo kila mmoja atakuwa ana uwezo wa kumudu bei na hapo ndipo tutakuwa tumeondokana na matumizi ya mbegu zisizokuwa bora," alisema Mlowe.

Naye Catheline Kabuge, mtaalamu wa uhawilishaji wa teknolojia za kilimo kwenye taasisi hiyo, alisema lengo la kuanzisha utaratibu huo ni kuwasaidia wananchi kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Alisema mfumo huo utawasaidia pia kuongeza kipato cha familia pamoja na kuwa na uhakika wa chakula na hivyo kuondokana na tatizo la udumavu ambalo linaikabili mikoa ya Nyanda za Juu Kusini licha ya kuwa inajitahidi kwenye uzalishaji.

Aliwataka vijana ambao walishiriki mafunzo hayo kuhakikisha wanayatumia vizuri mafunzo hayo, ili kuhakikisha wanaandaa mbegu ambazo watazitumia wao wenyewe pamoja na kuwauzia wakulima wengine.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema lengo la kuanzisha mafunzo hayo kwa vijana ni kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana kwa maelezo kuwa uzalishaji huo wa mbegu utasaidia vijana kujiajiri.

Alisema vilevile wanalenga kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula nchini kutokana na kwamba kutakuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji wa mbegu.

Alisema wanalenga kuwafundisha wakulima kuzalisha mbegu za mazao kama mtama, viazi, mahindi, maharage na mpunga ambayo ndiyo

# Wazee wa mila waombea uchaguzi mkuu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa mila katika mkoa wa Mbeya, wamefanya maombi maalumu ya kuliombea taifa, ili kuliepusha na majanga mbalimbali ikiwamo vurugu wakati huu wa kuelekea uchaguzi mkuu.

Walifanya maombi hayo juzi katika msitu wa machifu uliopo katika kata ya Igawilo jijini Mbeya, na waliongozwa na Mwenyekiti wa machifu wa Mkoa huo, Chifu Rocket Mwashinga.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa maombi hayo ambayo yaliambatana na matambiko, Chifu Mwashinga alisema maombi yao yalilenga kuzuia umwagaji damu wakati wa kampeni pamoja na kipindi chote cha uchaguzi.

Alisema kila Mtanzania aachwe achague kiongozi anayempenda bila kulazimishana, na kwamba asitokee mtu wa kumzuia Mtanzania mwenzake kutimiza haki yake ya kikatiba ya kupiga kura kwa maelezo kuwa matukio hayo ndiyo yanayosababisha vurugu.

"Mimi hapa nilipo nina miaka 77 na sijawahi kushuhudia umwagaji damu ndani ya taifa hili...haya maombi ambayo tunafanya hapa ni ya kuliombea taifa letu lisije likaingia kwenye machafuko ya aina yoyote wakati huu wa harakati za uchaguzi," alisema Mwashinga.

Chifu wa Mji Mdogo wa Mbalizi, Ezelina Mpoli, alisema wanachotaka ni uchaguzi wenye amani ambao utawezesha kupatikana kwa viongozi bora wa ngazi zote ikiwemo, rais, wabunge na madiwani ambao watasaidia kuleta maendeleo.

Alisema mbali na kuombea uchaguzi pia walikuwa wanafanya maombi ya kuzuia ajali katika maeneo mbalimbali nchini ambazo zimekuwa zikigharimu maisha ya watu.

Mpoli alisema maombi hayo na matambiko hayo pia yalilenga kuzuia matukio ya aina mbalimbali ambayo yanaweza yakapelekea umwagaji wa damu za watu.

"Sisi machifu pamoja na kwamba kila mmoja anaweza akawa na mtazamo wake wa kisiasa na akawa na mapenzi na chama chochote cha siasa, lakini inapokuja kwenye mambo ya kitaifa tunakuwa wamoja na tunaweka vyama vyetu pembeni," alisema Chifu Mpoli.

Naye Chifu George Lyoto, alisema vilevile maombi yao yalilenga kulinda mazingira kwa kuzuia watu ambao huwa wanafanya uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo.

Aliwaomba Watanzania kuwachagua viongozi ambao watasaidia kulinda mazingira kwa maelezo kuwa mazingira ndiyo uhai kutokana na kila shughuli kufanyika ndani ya mazingira.



Machifu wa Mkoa wa Mbeya, wakifanya maombi maalumu kuliombea taifa juzi, kwenye uwanja wa matambiko uliopo ndani ya msitu wa machifu kata ya Igawilo jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mitaji, vyama vya ushirika vyaongozeka kwa miaka 5

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MRAJISI wa vyama vya ushirika wa Mkoa wa Mbeya, Anjela Maganga, amesema katika kipindi cha miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano, sekta ya ushirika mkoani humo imeimarika ikiwamo kuongezeka kwa vyama pamoja na mitaji.

Akizungumza na Nipashe, Anjela, alisema mwaka 2015 wakati serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani, mkoa huo ulikuwa na vyama vya ushirika 406 pekee, lakini sasa una vyama 463 huku vyama vingine 68 vikiwa vimefutwa kutokana na kutofanya kazi kwa muda mrefu.

Alisema kati ya vyama hivyo, vipo vyama vikuu vitano, mradi wa pamoja mmoja, vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) 169, vyama vya ushirika wa wakulima (AMCOS) 185, vyama vya wafugaji 51, vyama vya wavuvi 19, vyama vya umwagiliaji 15 na vyama vingine 18.

Alivitaja vyama vikuu vya ushirika katika mkoa huo kuwa ni Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku, (CHUTCU), Chama Kukuu cha Ushirika Rungwe, Chama Kikuu cha Ushirika cha Kyela, Chama Kikuu cha Ushirikiano kati ya Mbeya na Ileje na Chama Kikuu cha wazalishaji wa maziwa.

"Mbali na idadi ya vyama vya ushirika kuongezeka katika kipindi hicho cha miaka mitano, pia mtaji wa vyama hivyo umeongezeka mara nne zaidi kutoka Sh. bilioni 16.58 mwaka 2015 mpaka kufikia zaidi ya Sh. bilioni 82," alisema Anjela.

Vilevile alisema serikali imefanikiwa kuboresha mfumo wa mauzo ya mazao ya wakulima kupitia vyama vya ushirika kwa mazao ya kahawa, tumbaku, chai na korosho mfumo ambao una faida zaidi kuliko ilivyokuwa awali.

Alisema mkoa huo umefanikiwa kuanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani kwa zao la kakao ambao umesaidia kupanda kwa bei ya zao hilo kutoka Sh. 1,500 kwa kilo mwaka 2015 mpaka Sh. 5,787, na kwamba zao hilo linauzwa kwa njia ya minada.

Mrajisi alisema pamoja na kwamba sekta ya ushirika ina maendeleo mazuri mkoani humo, pia kuna baadhi ya matatizo ambayo yanaikabili na kusababisha wakati mwingine kukwama.

Aliyataja baadhi ya matatizo hayo ni ubadhirifu wa mali za ushirika unaofanywa na baadhi ya viongozi na watendaji wa vyama wasiokuwa waaminifu na kwamba hali hiyo huwa inasababisha migogoro.

Pia anasema sekta hiyo inakabiliwa na tatizo la uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi, viongozi na watendaji kuhusu masuala ya ushirika hali ambayo husababisha baadhi ya vyama kushindwa kuendelea.

"Lakini kuna baadhi ya vyama vinakabiliwa na tatizo la kuwa na mitaji midogo kutokana na shughuli zao, tunaendelea kutoa elimu ili kuhakikisha vyama hivi vinatafuta vyanzo vingine vya mapato," alisema Anjela.

Alisema ofisi yake inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha sekta ya ushirika inakuwa endelevu na inakuwa na faida zaidi kwenye uchumi.

Alisema moja kati ya mikakati hiyo ni kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye vyama vya ushirika ili kujiridhisha kama vyama hivyo vinaendeshwa kwa kuzingatia sheria ya ushirika.

Aidha, alisema mkoa huo unakusudia kuhakikisha unatoa mafunzo ya mara kwa mara kwa viongozi, watendaji na wanachama wa vyama vya ushirika ili wawe na uelewa wa kutosha kuhusu uendeshaji wa ushirika kwa maelezo kuwa hilo ni miongoni mwa matatizo yanayodhoofisha sekta hiyo.



# Maalim Seif aahidi neema wakulima karafuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema endapo atapata ridhaa, atahakikisha wakulima wa viungo na karafuu wanakuwa huru kuuza mazao yao sehemu yoyote wanayotaka duniani.

Maalim Seif alisema hayo juzi katika kijiji cha Konde, Micheweni kisiwani Pemba ikiwa ni mwendelezo wa kampeni zake za urais kupitia chama hicho.

Alisema kazi ya serikali atakayoiongoza itakuwa kukusanya kodi ndogo, ili kuwafanya wakulima wapate faida kubwa na kuendeleza kazi yao hiyo kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Maalim Seif alisema serikali itawapatia mbinu na mazingira wakulima wa karafuu na bidhaa za viungo ili iwe ni njia ya kukuza uchumi wa Zanzibar.

"Tunataka kuwalea wakulima wetu wa bidhaa za viungo ili waweze kuitangaza Zanzibar katika masoko ya ulimwengu na wafanyabiashara za viungo waje Zanzibar kununua wenyewe," alisema Maalim Seif. Alisema hivi sasa wakulima wa bidhaa za viungo wamechoka sana kutokana na kuandamwa na kodi kubwa kila sehemu.

Maalim Seif ambaye ni Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Taifa, alisema kazi nyingine ya kufanya ni kuhakikisha Zanzibar inakuwa na mifugo bora na soko la uhakika.

Alisema atahakikisha huduma zote za mifugo zinapatikana ili kinachozalishwa kiwe na ubora katika masoko.

"Tutahakikisha viwanda vya dawa na vyakula vya mifugo yote vinapatikana hapa kwetu ili iwe rahisi wafugaji kuhudumia mifugo yao," alieleza Maalim Seif.

Alisema wafugaji wengi wa kuku visiwani Zanzibar wameacha kufanya kazi hiyo kutokana na upatikanaji wa dawa na vyakula Zanzibar kwa bei kubwa.

Mfugaji wa kuku katika kijiji cha Mtambile, Mkoa wa Kusini Pemba, Humud Muhammed Said, alisema ingalikuwa chakula cha kuku kinatengenezwa Zanzibar wafugaji wangepata tija katika mifugo.

Alisema kwa mfano kwa siku yeye anahitaji matumizi ya magunia mawili na nusu kwa siku, analazimika kununua moja kwa Sh. 50,000.



Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu Zanzibar, Idd Khamis Haji (katikati), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) Tanzania Bara, Abdul-Razaq Badru (kulia) wakati wa ziara ya kikazi katika Ofisi za HESLB zilizopo Tazara jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Meneja Mikopo wa ZHESLB, Aboud Iddi Khamis.

# Dk. Mwinyi ahamasisha mazao ya viungo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wakulima Pemba kujikita katika kilimo cha mazao ya viungo ambacho soko lake ni kubwa.

Alisema endapo atachaguliwa kuwa rais, wakulima wajitayarishe na uwekezaji wa viwanda vitakavyoongeza thamani ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Akizungumza jana na makundi ya wakulima mbalimbali Chakechake kisiwani Pemba, Dk. Mwinyi alisema mazao ya viungo ndiyo mkombozi wa wakulima na kupiga hatua kubwa ya kiuchumi. Mgombea huyo alisema mazao ya viungo kama vile pilipili manga, pilipili hoho, pilipili kichaa, hiliki na mdalasini hivi sasa bei yake ni kubwa katika soko la dunia ikiwamo katika bara la Asia. Alisema ardhi ya kisiwa cha Pemba ni nzuri yenye rutuba na kuruhusu kuwapo kwa ukuaji wa mazao mbalimbali yenye tija na soko kwa wakulima yakiwamo mazao ya viungo.

"Wakulima wa kisiwa cha Pemba nawaombeni ongezeni kasi ya kulima mazao ya viungo ambayo kwa sasa soko lake lipo kubwa la uhakika katika nchi za Ulaya na Asia," alisema.

Pia aliwataka kuendelea na juhudi zao za kulima karafuu kutokana na kuongezeka kwa mahitaji yake ya usarifu kwa kupata bidhaa ya mafuta kutokana na makonyo yatokanayo na zao hilo.

Dk. Mwinyi aliwapa habari nzuri za juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuongeza viwanda vya kusarifu bidhaa inayotokana na malighafi ya karafuu yakiwamo makonyo. Alisema kuwapo kwa viwanda hivyo kwa kiasi kikubwa kutaongeza pato la wakulima na kujipatia fedha nyingi ambazo zitatokana na juhudi zao binafsi za kuzalisha bidhaa za aina hiyo.

Mgombea wa urais wa Zanzibar kupitia CCM, yuko Pemba akitembelea makundi ya watu mbalimbali kutaka kujua matatizo yao na njia ya kuyapatia ufumbuzi kama atachaguliwa kuwa rais wa Zanzibar.

## Mgombea aonya kuhusu uchochezi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya UPDP, Hamad Mohammed Ibrahim, amewataka wananchi na wanachama wa chama hicho kuwa makini katika kipindi hiki cha kampeni kwa kutokufuata maneno ya watu ambayo yatasababisha kuvunjika kwa amani ya nchi.

Aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni za chama hicho uliofanyika uwanja wa Garagara, Wilaya ya Magharibi A, Unguja.

Hamad aliwataka wananchi kuwa waangaalifu wanaposikiliza sera za wagombea na kutokufuata maneno ya uchochezi ambayo husababisha migogoro katika nchi kwa sababu kuna maisha baada ya uchaguzi.

Aliongeza kuwa ikiwa watakubali kulishwa maneno ya uchochezi na kuwa na jazba za kisiasa inaweza kuleta athari kubwa kwa wananchi hivyo aliwataka kulinda amani iliyopo.

"Sisi UPDP tunajua kuna maisha baada ya uchaguzi kwa hiyo wananchi hatutakiwi kwa namna yoyote kulishwa maneno ya uchochezi," alisema Hamad.

Aidha, alisema akifanikiwa kupata nafasi ya urais wa Zanzibar, atahakikisha anaimarisha rasilimali za ardhi ili kudumisha maendeleo nchini.

Naye mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya chama hicho, Twalib Ibrahim Kadege, alisema miongoni mwa vipaumbele vya chama chao ni kuhakikisha rushwa inaondoka na kuimarisha sekta ya afya.

"Hii nchi ina tatizo la rushwa kwa muda mrefu UPDP ikiingia madarakani itaondosha rushwa na atakayekamatwa na rushwa atapigwa bakora mia moja na jela miaka 100," alisema Twalib.

Kwa upande wake mgombea mwenza wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Ramadhan Ali Abdallah, alisema Tanzania ni nchi yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha bidhaa, hivyo UPDP itaifanya kuwa kitovu cha biashara.

"Hakuna sababu ya kuchukua bidhaa kutoka nje wakati tuna uwezo wa kuzalisha wenyewe," alisema Ramadhan.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Feisal Al Sultan** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **RAV 4 yenye namba ya usajili T777 AEL** iliyotolewa na Mamlaka ya mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **TRM/RB/1401/2020.**

115904802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;279/2020**

**Ombi la RAMADHANI IDDI SAIDI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SOPHIA COSMAS MBAWALA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/09/2020.

Tarehe 17/9/2020
Sahihi ya Hakimu
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115906102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;278/2020**

**Ombi la HELENA M.KWAMBA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MACDONALD KWAMBA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/09/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

115906202

---

**IN RESIDENT/DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**CIVIL CASE NO 17 OF 2020**

**JOHN FELIX KAWISHE……………………PLAINTIFF**

**VERSUS**

**STEVENS ELISHA CHIDOLE…………………DEFENDANT**

**TO: STEVENS ELISHA CHIDOLE**
**BOX 3147 DODOMA**

Whereas your attendance reguired to WIT AS THE 1ST DEFENDANT in the above suit, you are hereby reguired (personally) to appear before this court on the 23rd day of September, 2020 AT 8:30 O clock
If you fail to comply with this order without lawful excuse. you will be subject to the consequences of non-attendance laid down in Rule 12 of Order XVI of the Code of Civil Procedure.1966 CAP 33 R.E.2002.
Given under my hand and the seal of the Court. This 14th day 09 of 2020.

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE IN DODOMA DISTRICT

115905402

---

## KUBADILISHA JINA



Mwenye picha hapo juu anatangaza kubadilisha jina lake la awali ambalo ni **SAKINA MUSTAFA HASHAM** na kwa sasa atatambulika kama **SAKINA ALIRAZA MEGHJI** kwa mujibu wa sheria. **RD/OPT/20/43/640**

115905902

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANGEL SAFARI SANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA IST YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 880 DHN.** Chassis namba **NCP600116087.** Engine namba **2NZ2848356.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KW/K/B.I/I/VOL.253.**

115904702

---

**JAMUHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA (MCA:63)**

**Mahakama ya mwanzo ya Mjini Tanga Wilaya Tanga**

**MADAI NAMBARI: 18 ya 2020**

**Mdai ALFRED GIBSON SIWELWA**

**Mdaiwa: UPENDO MARTIN MNZAVA**

**Kwa: UPENDO MARTIN MNZAVA**

Kwa kuwa mdai/mdaiwa ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba/eleza hapa Habari za madai TALAKA

Kwahiyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudi uria binafsi katika mahakama hii siku ya Jumanne tarehe 22/09 saa 2:30 asubuhi alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/ wen una hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo Angalia kama hukuhudhuria/ hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu , mahakama ikithibitisha kama umepokea/ mmepokea kuitwa shauri hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ mmeshindwa
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 15/09/2020

……………………………
**Hakimu wa mahakama ya mwanzo**

115905302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NA: 116/2020**

**MDAI: ADELA KARUNGI ISHUZA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: ERIBART ADOLF WA NYANKUMBU (W) GEITA**

**AMRI:** Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 24/09/2020 saa 2:30 asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo tarehe 03/09/2020.

HAKIMU

115904602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA:………….**

**Mdai: ROSE LUCAS**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: MELIKZEDEK EIZER**

**Kwa: MELIKZEDEK EIZER**

**Ombi la mdai/Muombaji/Msimamizi ROSE LUCAS Madai ya TARAKA NA MGAWANYO WA MALI.**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 24 mwezi 09 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 16 mwezi 09 mwaka 2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

115904902

---

## KUBADILISHA JINA



Mwenye picha hapo juu anatangaza kubadilisha jina lake la awali ambalo ni **ZAINABU JAFFER LADHA** na kwa sasa atatambulika kama **ZAINABU SHABBIR YUSUFALI MEGHJI** kwa mujibu wa sheria. **RD/OPT/20/49/155**

115905902

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FREDRICK ARBOGAST CHAMI.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SUNLG** yenye namba za usajili **MC 547 AUT.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/673099/2020.**

115905702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo KINGOLWIRA**

**Usimamizi wa mirathi No; 16/2020**

**Ombi la EMANUEL IKUNDAEL KAFUI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ELIHAIKA ELIHAKIMU KAFUI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/09/2020.

Sahihi ya Hakimu
MAHAKAMA YA MWANZO KINGOLWIRA MOROGORO

115905002

---


**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Nchimbi awaagiza wananchi maombi

Na Edina Alex, SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, amewakumbusha wananchi kutambua kuwa Mungu yupo kwa kuwa amewaepusha na majanga mengi likiwamo la ugonjwa hatari wa corona.

Dk. Nchimbi aliyasema hayo juzi alipoalikwa kufungua mkutano wa injili ulioanza juzi mjini hapa, ulioandaliwa na mwinjilisti wa kimataifa Dk. Egon Falk.

Aliwaambia kuwa Rais John Magufuli kutokana na kutambua kuwa Mungu yupo alitangaza maombi ya siku tatu kwa nchi nzima, ili kuwaepushia ugonjwa huo Watanzania na Mungu alisikia maombi hayo.

"Haiwezekani Mungu huyu aliyetuondolea corona halafu eti tuendelee kusema Singida ni maskini, Tanzania ni maskini wakati kuna rasilimali, haiwezekani," alisema Dk. Nchimbi.

Pia, aliwaasa wananchi wasitenganishwe na uchaguzi na badala yake waungane bila kuangalia madhehebu yao, ili kuijenga nyumba ya Bwana, ambayo ni Mkoa wa Singida na Tanzania kwa ujumla.

"Katika uchaguzi wa mwaka huu tuende tukabariki sio kuchinja, vitambulisho tulivyonavyo tukavitumie katika kubariki na sio kuchinja kama wanavyosema wengi," alisema.

Kwa upande wake Mwiinjilisiti Dk. Egon aliwashukuru viongozi wa serikali ya Tanzania kwa kuruhusu mikutano ya injili kufanyika hadharani, bila kuzuiwa na kiongozi yeyote.

"Takribani miaka 46 sasa niko hapa Tanzania nikihubiri neno la Mungu, sijawahi kuzuiwa na kiongozi yeyote, sijawahi kuona kiongozi yeyote wa nchi duniani akitangaza siku tatu za maombi ya kufunga ni Tanzania pekee, Mungu awabariki sana Watanzania," alisema Egon na kuongeza:

"Ulaya watu wamebarikiwa wamekuwa na maendeleo, lakini hawamtambui Mungu, nawaomba Watanzania mkipata maendeleo msimsahau Mungu."

**Haiwezekani Mungu huyu aliyetuondolea corona halafu eti tuendelee kusema Singida ni maskini, Tanzania ni maskini wakati kuna rasilimali, haiwezekani.**

# RITA yaja na kampeni 'One Stop Jawabu'

Na Mwandishi Wetu

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Temeke, imeandaa kampeni inayojulikana 'One stop Jawabu' maalum kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali ikiwamo vyeti vya kuzaliwa, kuandika wosia, mirathi na kuitunza pamoja mambo mengine ya kisheria.

Katika kampeni hiyo ambayo ilizinduliwa rasmi Septemba 14, Mbagala itaendelea mpaka Septemba 20, kabla ya kuhamia katika viwanja vya Mwembe Yanga, Tandika, jijini Dar es Salaam.

"Tumekuwa hapa tangu tarehe 14 mwezi huu siku ya uzinduzi tukiwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, ambaye alisisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi ili kutumia fursa hiyo vizuri,"

"Kuanzia tarehe 22 mpaka 28, mwezi huu tutakuwa katika viwanja vya Mwembe Yanga, Tandika lengo ni kuendelea kuwafikia zaidi wakazi wa Dar es Salaam na ndio maana tunatumia viwanja vya wazi ili waweze kupata huduma hiyo wakiwa kwa wingi," alisema Jafari Malema, Ofisa Habari wa RITA.

Pia ofisi ya Mkuu wa Wilaya Temeke, ambao ndio wadau walioshirikiana na RITA kuhakikisha kazi hiyo linafanikiwa, Mkuu wa wilaya hiyo, Godwin Gondwe, alisema shughuli kama hiyo aliifanya akiwa katika Wilaya ya Handeni na alifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Niliendesha Handeni kwa kushirikiana na RITA na lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa hivyo nanyi wakazi wa Temeke msilaze damu huduma sasa iko karibu yenu jitokezeni ili mpate huduma mbalimbali za RITA zikiwamo vyeti vya kuzaliwa," alisema Gondwe.

Alisema kuwa vyeti vya kuzaliwa vina umuhimu mkubwa hasa kupata cheti cha utambulisho wa taifa, mikopo vyuoni na masuala mbalimbali ya ajira.

Kwa Mujibu wa Malema mpaka sasa watoto 2,700 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa huku kazi hiyo ikiwa inaendelea.



Meza za wafanyabiashara zikiwa zimeachwa ndani ya mtaro, kando ya Barabara ya Bagamoyo eneo la Tegeta, jijiji Dar es Salaam jana, hali ambayo inaweza kuchafua mazingira. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wajifunza hukumu uhalifu wanyamapori

Na Mwandishi Wetu

WATUMISHI 70 wa Mahakama Kanda ya Kusini mwa Tanzania wamemaliza mafunzo ya kuimarisha mashtaka na hukumu za uhalifu wa wanyamapori.

Mafunzo hayo yalifadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA), Shirika la Wanyamapori Duniani (WWF) na TRAFFIC. Mafunzo hayo yalitekelezwa kama sehemu ya mradi wa USAID wa Kutunza Mazingira, Uhifadhi, na Utalii (PROTECT).

Washiriki walijifunza juu ya sera na sheria za wanyamapori, uchunguzi na mashtaka ya uhalifu wa wanyamapori, na ushirikiano baina ya mashirika kutoka kwa Jaji mstaafu, Robert Makaramba na Linah Clifford, Ofisa Sheria kutoka TRAFFIC Afrika Mashariki.

"Kwa kuboresha uwezo wa mahakama na watekelezaji wa sheria kuchunguza vizuri na kuhukumu kesi za uhalifu wa wanyamapori, tunatarajia kuzuia wahalifu kuendelea kusafirisha wanyama," alisema Thadeus Binamungu, Msimamizi mradi, USAID PROTECT.

Ongezeko la mahitaji ya bidhaa zitokanazo na wanyamapori, hasa bara la Asia, linatishia wanyama na mimea nchini Tanzania, kama vile faru mweusi na kakakuona wa kiafrika kutoweka.

Kati ya 2009 na 2014, Tanzania ilipoteza asilimia 60 ya idadi ya tembo kutokana na ujangili wa wanyamapori na usafirishaji haramu.

"Serikali ya Marekani imeazimia kuzuia usafirishaji haramu wa wanyama pori barani Afrika na ulimwenguni kote," alisema Terhi Majanen, Mkurugenzi wa Ofisi ya Ukuajiwa Uchumi ya USAID nchini Tanzania.

"Kama muungano baina ya mashirika, tunayo furaha kusaidia washirika wetu katika Serikali ya Tanzania kufikia malengo yao ya kupunguza uhalifu wa wanyamapori na kukuza haki."

Biashara haramu ya wanyama pori inaendeshwa namitandao ya kihalifu na minyororo ya thamani ambayo inahitaji utashi wa hali ya juu wa kisiasa, uratibu, ushirikiano, na ushiriki thabiti wajamii kuisambaratisha. Kila mwaka, biashara haramu ya wanyama pori huondoa mabilioni ya Dola za Marekani za mapato ya kitaifa kutoka nchi zinazo endelea kwenda kwa wahalifu na mitandao inayohusika na uhalifu huo.

Mafunzo hayo, yaliyoanza Julai, yalileta pamoja wadau na washirika wa nje kama vile huduma za uvuvi na wanyama pori ya Marekani, Taasisi ya Wanyamapori ya Afrika, Kituo cha Sheria cha Mazingira cha Jumuiya ya Kimataifa ya Kuhifadhi Maeneo Asilia, Mamlaka ya Wanyamapori ya Uganda, na Mahakama ya Uganda. Wawakilishi kutoka kwa mashirika haya waliwapa washiriki uelewa mpana wa majukumu yao katika kupambana na uhalifu wa wanyamapori, upungufu katika sheria ya utekelezaji wa wanyamapori na udhaifu wa sasa katika uchunguzi na mashtaka.

Washiriki pia walisikia kutoka kwa majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Huduma ya Mashtaka ya Kitaifa, Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, TRAFFIC na Wizara ya Maliasili na Utalii.

# WERNER: LAMPARD ALINIVUTIA CHELSEA




**LONDON,** England

TIMO Werner amesema mtazamo wa Frank Lampard kwa namna anavyotaka Chelsea iwe, ndio sababu ya yeye kusaini kwa miamba hao wa Ligi Kuu England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, alijiunga na Blues hao kwa ada ya pauni milioni 47.5 kutoka RB Leipzig, kipindi hiki cha majira ya joto na alicheza mechi yake ya kwanza Jumatatu, wakati wakiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Brighton and Hove Albion.

Werner mwenye umri wa miaka 24, amesema hakusita kujiunga na Chelsea baada ya Lampard kubainisha namna gani atafiti kwenye mfumo wake.

"Alinipigia mara nyingi," alisema Werner akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulijadiliana mambo mengi, alinitumia ujumbe mfupi mara nyingi na baadhi ya video na kuonyesha staili anayotaka timu yake icheze.

"Hivyo, kwangu mimi, hayo yote yalikuwa muhimu kuyajua na nikaamua kwa moyo mmoja kujiunga na Chelsea. "Nilipenda kuichezea Leipzig na mambo mengi yalikwenda vizuri, lakini kwa uhakika kabisa niliamua kuangalia changamoto nyingine, ili kukua zaidi kiuchezaji."

# Messi afunga kwa mara ya kwanza tangu arejee

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi aliifungia kwa mara ya kwanza Barcelona, tangu atangaze uamuzi wa kubakia katika klabu hiyo, wakati wakishinda mabao 3-1 dhidi ya Girona, kwenye mchezo wa kirafiki.

Nahodha huyo wa Blaugrana alifunga mabao mawili kwenye ushindi huo, ambapo sasa amebakiwa na mwaka mmoja wa kukaa hapo Camp Nou, baada ya jaribio lake la kutaka kuondoka kushindikana.

Messi alikuwa akihusishwa na mpango wa kutua kule Manchester City, lakini aliamua kusitisha mpango wa kuondoka Barca baada ya kushindwa kuafikiana na klabu yake hiyo.

Nyota huyo anayevaa jezi namba 10, alirudi kwa mara ya kwanza kuichezea timu yake inayonolewa na Ronald Koeman, kwenye mchezo wa kiurafiki dhidi ya Gimnastic Jumamosi iliyopita, lakini hakufunga.

Lakini Messi katika mchezo huo wa juzi alifunga mara mbili, huku bao lake la kwanza akifunga kwa mguu wa kulia, kwa shuti kutoka umbali wa yadi 20.

La pili alifunga kwa shuti pia, baada ya Philippe Coutinho kuiweka mbele Barcelona kwa bao la kwanza.

Messi alitolewa dakika ya 63 na nafasi yake kuchukuliwa na Ousmane Dembele na sasa wanasubiria mchezo wa mwisho wa kirafiki, dhidi ya Elche kabla ya kuanza kampeni ya Laliga kwa kuwavaa Villarreal Septemba 26, mwaka huu.







# *Neymar afungiwa michezo miwili*

**PARIS,** Ufarasa

NEYMAR amefungiwa kucheza mechi mbili baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu, wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Ufaransa kati ya timu yake ya Paris Saint-Germain na Marseille.

PSG walichezea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa wapinzani wao wa jiji moja, Marseille hapo Jumapili mchezo ambao ulimalizika kwa vurugu kubwa na wachezaji watano kulimwa kadi nyekundu.

Mshambuliaji huyo ghali zaidi duniani, alimpiga ngumi nyuma ya kichwa mlinzi, Alvaro Gonzalez na kuonyeshwa kadi nyekundu.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alidai kwamba, alitamkiwa maneno ya ubaguzi wa rangi Alvaro na hivyo kuamua kumtia ngumi.

Matokeo ya kamati ya nidhamu yalitangazwa jana na Neymar akafungiwa kucheza mechi mbili.

Layvin Kurzawa ambaye pia alihusika kwenye vurugu hizo, amefungiwa mechi sita, huku Leandro Paredes akifungiwa mechi mbili.

# De Boer kumrithi Koeman Uholanzi

**AMSTERDAM,** Uholanzi

UHOLANZI inatajwa inakaribia kukamilisha mchakato wa kumwajiri beki wake wa zamani wa Timu ya Taifa, Frank de Boer kurithi mikoba iliyoachwa na Ronald Koeman, imefahamika.

Kikosi cha Timu ya Taifa ya Uholanzi kimekuwa bila ya kocha tangu Agosti, mwaka huu baada ya Koeman kuondoka na kujiunga na Barcelona.

Dwight Lodeweges alikuwa akikaimu nafasi hiyo, lakini De Boer anatarajiwa kupewa mkataba wa kudumu kwa kukiongoza kikosi hicho, RTL Nieuws imeandika.

Uholanzi wanatarajia kumtangaza kocha huyo mpya kabla ya mapumziko ya kujiandaa na mechi ya kirafiki itakayochezwa baadaye mwezi ujao.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 50, aliwahi kuzifundisha Ajax, Inter Milan na Crystal Palace, huku akiichezea Uholanzi mechi 112 katika kipindi cha kuanzia 1990 hadi 2004.

Kwa sasa De Boer alikuwa hana timu baada ya kuondoka kwenye kikosi cha Atlanta United kilichokuwa kinashiriki Ligi Kuu ya Marekani, mapema majira ya joto mwaka huu.

Koeman, ambaye amerithi mikoba ya Quique Setien katika kikosi cha Nou Camp mwezi uliopita, aliiongoza vema Uholanzi kwa muda wa miaka miwili na alifanikiwa kumaliza katika nafasi ya pili kwenye mashindano ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya mwaka jana.



# TUCHEL AMTAJA MBAPPE WAKIJIANDAA KUIVAA NICE




**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Mkuu wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel ana matumaini ya kumtumia Kylian Mbappe kwenye mchezo wa Jumapili dhidi ya Nice.

Mbappe bado hajaichezea PSG kwa msimu huu wa 2020-21, baada ya kupimwa na kukutwa na virusi vya corona wakati akiwa na kikosi cha timu ya taifa ya Ufaransa, mapema mwanzoni mwa mwezi huu.

PSG ilipoteza mechi zake mbili za ufunguzi wa ligi hiyo, lakini walipata ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo wao wa dhidi ya Metz, Jumatano.

Tuchel amesema ana matumaini kumtumia Mbappe ambaye alifunga mabao 30 katika msimu wa 2019-20, kwenye mchezo dhidi ya Nice.

"Kylian anajisikia vizuri. Hana dalili zozote," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Alikutwa na virusi vya corona, lakini hakuonyesha dalili zozote. Kwa sasa anajisikia vizuri. Alikuwa anafanya mazoezi ya peke yake.

"Pengine pia tutaweza kuwatumia pia Angel (Di María), Marquinhos na Mauro Icardi."

# *Jose ajitetea mabadiliko ya Alli*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amesisitiza "hakuna ishu yoyote" juu ya uamuzi wake wa kumtoa nje, Dele Alli katika kipindi cha pili wakati Tottenham ikichezea kichapo kutoka kwa Everton.

Spurs ilianza msimu mpya wa Ligi Kuu England kwa kichapo Jumapili, kwa bao lililofungwa na Dominic Calvert-Lewin kwa kichwa.

Alli alicheza kwa dakika 45 tu za kipindi cha kwanza, kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Moussa Sissoko.

Hata hivyo, Mourinho alisema uamuzi wa kumtoa kipindi cha pili ilikuwa ni sehemu ya mchezo na sio kutokana na uhusiano wake na Alli kulegalega.

"Mabadiliko ya kipindi cha pili haikuwa mara ya kwanza katika maisha yangu ya ukocha, na haiwezi kuwa ni mara ya mwisho," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Mara ya mwisho nilifanya hivyo kwa Eric Dier kwenye mchezo dhidi ya Olympiacos wakati nilipomtoa dakika ya 25 au 30. Ninapofanya mambo haya huwa nafanya kwa ajili ya timu na sio dhidi ya mchezaji.

"Kuna nyakati maamuzi yangu yalionekana kuwa na maana na ni kwa sababu ya kimchezo tu na si vinginevyo."

Ali na Mourinho wanaripotiwa kutokuwa kwenye mahusiano mazuri na anatajwa kwamba anataka kufanywa mbadala wa Gareth Bale, ambaye anataka kurudi Spurs baada ya kutokuwa na nafasi katika kikosi cha Real Madrid.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GARETH BALE AREJEA RASMI TOTTENHAM

## Mourinho atajwa kusimamia uhamisho wake wa winga huyo wa Wales kurejea Spurs...

**LONDON,** England

HATIMAYE juzi usiku, Gareth Bale alikamilisha mchakato wa kurejea Tottenham, uhamisho ambao umefanyiwa kazi na Jose Mourinho.

**Winga huyo wa Timu ya Taifa ya Wales amekubali kurejea Spurs kwa mkataba wa mwaka mmoja huku gazeti la Sportsmail likifahamu dili hilo limefanyika kwa thamani ya pauni milioni 13, huku sehemu ya malipo hayo yakilipwa na Real Madrid.**

Hata hivyo hakuna dalili ni lini Tottenham, ambayo ilitarajia kuivaa Lokomotiv Plovdiv jana katika mechi ya Ligi ya Europa League itamtangaza winga huyo, lakini huenda wanasubiri mchakato kamili kukamilika na kusainiwa.

Bale amefanikiwa kurejea London Kaskazini ikiwa imepita miaka saba tangu alipoondoka na kununuliwa na Madrid kwa dau lililoweka rekodi ya dunia la pauni milioni 90, lakini ni Mourinho ndiye anatajwa kusimamia uhamisho huo, zikiwa ni siku chache baada ya kufungwa bao 1-0 na Everton Jumapili iliyopita.

Usajili wa Bale unatajwa kuwa tofauti na mchakato wa kuwanasa nyota wengine akiwamo beki wa kushoto, Sergio Reguilon kutoka Real Madrid ambaye anahusishwa kuwindwa na Manchester United.

Reguilon tayari ameshatua London na endapo atafaulu vipimo vya afya atasaini mkataba wa miaka mitano ambao utaikamua Tottenham kiasi cha pauni milioni 27.

"Nimejaribu kumsajili nyota huyo akitokea Real Madrid jambo ambalo lilikuwa haliwezekani wakati mimi nilipokuwa pale," Mourinho alisema juzi Jumatano alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Bale alikuwa kipenzi cha mashabiki wa Spurs baada ya kufanikiwa kufunga mabao 56 na kutoa pasi za mwisho 58 kwenye mechi 203 alizocheza.

Msimu wa 2012/13 alitangaza kuwa Mchezaji Bora wa Mwaka wa Tottenham na pia alitwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Kulipwa (PFA), Mchezaji Bora Chipukizi wa PFA na mshindi wa tuzo ya Mchezaji Bora wa msimu wa Ligi Kuu England.

Alikuwa ni mchezaji mwenye kiwango cha juu kwenye Ligi Kuu England na kuifanya Real Madrid kuvutiwa kumsajili baada ya dirisha la usajili kufunguliwa na kuungana na Cristiano Ronaldo hapo Santiago Bernabeu. Bale alikuwa hana mahusiano mazuri na kocha wake, Zinedine Zidane kule Real Madrid huku pia akihusishwa na mpango wa kuuzwa.

Klabu ya Manchester United ilikuwa pia ikihusishwa na mpango wa kumsajili nyota huyo.

## ZISIKUPITE

### ALLI KUMPISHA BALE

KIUNGO wa Tottenham Hotspur, Dele Alli, ameamua kuondoka katika kikosi cha timu hiyo na kutoa nafasi kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale (31), kurejea klabuni hapo akitokea Real Madrid. ***(Mail)***

### SERGIO ANUKIA SPURS

BEKI wa kushoto wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania, Sergio Reguilon (23), ametua katika viwanja vya mazoezi vya Spurs kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya afya na baadaye kukamilisha mchakato wa usajili ambao thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 25. ***(Evening Standard)***

### TOMORI KUTUA EVERTON

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti anataka kumsajili beki wa Chelsea na Timu ya Taifa England, Fikayo Tomori (22), lakini atalazimika kuwatema baadhi ya wachezaji walioko Goodison Park, akiwamo kiungo wa Iceland, Gylfi Sigurdsson (31) na kiungo wa England, Fabian Delph (30). ***(Times - subscription required)***

### GIMENEZ ATAJWA CITY

MANCHESTER City iko tayari kumwania beki wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Uruguay, Jose Gimenez (25), kama Napoli itakataa kupunguza ada ya kumuuza beki wake wa kati Msenegal, Kalidou Koulibaly (29). ***(Guardian)***

### PARTEY AIVURUGA ARSENAL

KIUNGO mkabaji wa Atletico na Timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Partey (27), ni mmoja wa nyota wanaotakiwa na Arsenal lakini klabu yake ya Hispania inasisitiza itakuwa tayari kumuuza endapo timu inayomhitaji itatoa kiasi cha pauni milioni 45. ***(Football. London)***

### TRAORE ANUKIA UNITED

MABOSI wa Manchester United wanajiandaa kunasa saini ya winga raia wa Ivory Coast, Amad Traore (18), akitokea Atalanta nchini Italia. ***(Manchester Evening News)***

### KLOPP ATAKA WAWILI

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, huenda akasajili wachezaji wapya wawili au mmoja kabla ya dirisha la usajili halijafungwa ifikapo Oktoba 5, mwaka huu. ***(The Athletic - subscription required)***

### UNDER AKARIBIA LEICESTER

LEICESTER City inakaribia kukamilisha usajili wa winga wa Roma na Timu ya Taifa ya Uturuki, Cengiz Under, ambaye ana umri wa miaka 23. ***(Telegraph - subscription required)***

### GENOA YAMNASA ROSE

BEKI wa kushoto wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Danny Rose (30), anajiandaa kujiunga na klabu ya Serie A ya Genoa baada ya kukosa namba kwenye kikosi cha Spurs. ***(Mirror)***

### KOEMAN AMTAKA GARCIA

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amependekeza klabu hiyo ya La Liga kutomsajili beki wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Hispania, Eric Garcia, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

## Watatu Biashara kuikosa Simba SC

**NA Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Biashara United kinatarajia kuwasili jijini, Dar es Salaam leo usiku tayari kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini bila ya nyota wake watatu.

Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, alisema anatarajiwa kuwakosa nyota wake watatu ambao ni Gerald Mdamu, Joseph Ziwa na Abdul Mangalo kutokana na kuwa majeruhi.

"Wachezaji wote wanaendelea vizuri, isipokuwa hao niliokutajia, tumefanya vema maandalizi ya kukutana na Simba, hatumhofii mchezaji hata mmoja," alisema Baraza.

Alieleza licha ya kufungwa mabao 2-0 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Mbao FC iliyochezwa juzi, mchezo huo umewasaidia kuwaunganisha wachezaji wake wapya na wa zamani ambao wanaitumikia timu hiyo.

"Ninayafanyika kazi mapungufu yote niliyoyaona, napenda niseme kila mchezaji ana morali ya hali ya juu ya kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, wachezaji wananipa matumaini kwa kile wanachokifanya, wanafuata vizuri maelekezo yangu," alisema kocha huyo.

Aliongeza licha ya mchezo huo kutarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani, nyota wake wamejipanga kupambana kuhakikisha hawapotezi na tayari wameshawachunguza wapinzani wao katika michezo yao iliyopita.

## Kriketi Tanzania yazidi kujijenga

**Na Adam Nyangasa,** TUDARCo

TIMU ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 19 ya kriketi inaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kupeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano ya Afrika, imeelezwa.

Tanzania ndiyo mwenyeji wa mashindano hayo yatakayofanyika Januari, mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Steven Tikolo, alisema anafurahishwa na viwango ambavyo vijana wake wanavyo na anaamini mazoezi yanayoendelea yanawaimarisha vizuri.

Tikolo alisema hadi kufikia Desemba, mwaka huu, wachezaji wake watakuwa wameimarika na wako tayari kwa mashindano.

Alisema anaendelea kufanyia kazi sehemu zenye mapungufu kwa kuwapa mbinu mbadala ili kujiweka imara na tayari kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

"Tunajaribu kuboresha idara zote za mchezo ambazo ni pamoja betting, balling na fielding, lakini upande ambao tunaufanyia zaidi kazi ni betting, kwa sababu hapo awali timu haikua vizuri sehemu hiyo," alisema Tikolo.

Kocha huyo aliongeza vijana wake wanacheza michezo mbalimbali ya kujipima kwa lengo la kujijenga na wakati wote wameonyesha viwango vizuri na vinavyoonyesha wako tayari kupambana.

# LA LIGA, M-BET KUKUZA VIPAJI, MAKOCHA NCHINI

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubahatisha ya M-Mbet na waendeshaji wa Ligi Kuu Hispania maarufu La Liga San Tander wameingia makubaliano ya kuendeleza vipaji mbalimbali nchini Tanzania.

**Kampuni hizo mbili zimesaini mkataba wa miaka mitatu, ambapo mbali ya kuendesha mafunzo ya soka kwa vijana, pia watafanya mafunzo kwa makocha na waamuzi kwa kutumia wataalamu wa La Liga.**

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema timu wanaoyoidhamini ya KMC ambayo inashiriki Ligi Kuu Bara, nayo itafaidika na makubaliano hayo ambayo lengo lake kubwa ni kuendeleza mpira wa miguu nchini.

Mushi alisema safari ya M-bet ya kukuza soka hapa nchini ilianza miaka miwili iliyopita na sasa wameamua kutanua wigo kwa kujipanga kutoa mafunzo kwa wachezaji wenye umri kuanzia miaka 18.

"Lengo hapa ni kuwapa faida wateja wetu ambao ndiyo nguzo pekee katika maendeleo ya kampuni yetu, mara baada ya Ligi ya Hispania kumaliza kuruhusu watazamaji na mipaka kufunguliwa, wateja wetu wataweza kubashiri na washindi watakwenda kuangalia ligi hiyo," alisema Mushi.

Aliongeza ushirikiano huo utasaidia kukuza vipaji na kutimiza ndoto za vijana ambao ndiyo nguzo kubwa ya maendeleo ya soka nchini.

Mwakilishi wa La Liga San Tander wa Tanzania, Alvaro Paya, alisema wamefurahi kuingia makubaliano na M-Bet na kuwa washirika wa pili baada ya klabu ya Yanga.

Paya alisema lengo la La Liga ni kuhakikisha mpira wa Tanzania unasonga mbele na wamegundua kuna vijana wengi wenye kuhitaji kuendeleza vipaji vyao, lakini wanakosa njia ya kufikia katika ndoto zao.




Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi (kushoto), akizungumza baada ya kusaini mkataba wa miaka mitatu na waendeshaji wa Ligi ya Hispania, La Liga San Tander kwa ajili ya kuendeleza wachezaji, makocha na waamuzi wa soka nchini. Kulia ni mwakilishi wa La Liga, Alvaro Paya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Manara wa kwanza kulipa faini TFF*

**Na Adam Fungamwango**

OFISA Habari wa Simba, Haji Manara, amekuwa wa kwanza kulipa faini ya Sh. milioni tano alizohukumiwa na Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imefahamika.

Mapema wiki hii, Kamati ya Maadili iliwatia hatiani Manara, Mjumbe wa Bodi ya Klabu ya Simba, Zacharia Hanspope na Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli, kila mmoja akiwa na makosa tofauti, kulipa kiasi hicho cha fedha, katika kipindi cha kesi ya mchezaji raia wa Ghana, Bernard Morrison dhidi ya Yanga ilipokuwa ikisikilizwa.

Juzi picha zilianza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii zikimwonyesha Manara akipeleka 'burungutu' la fedha katika ofisi za TFF na kuzikabidhi kwa mhasibu wa shirikisho hilo, ambaye aliahidi kuzipeleka benki na kumpatia risiti mshtakiwa huyo.

Manara alisema ameamua kulipa faini hiyo kwa sababu yeye na klabu yake hawakutaka kukata rufani na wameridhishwa na uamuzi huo wa kamati.


"Sikulipa kwa sababu ya kiburi, maana inaweza kutafsiriwa hivyo, ila ni kuleta amani kwenye mpira wetu, lakini kuridhika na kile ambacho kamati imeamua. Tunaamini kwa kufanya hivi, tutatengeneza mpira wetu kwa misingi ya kinidhamu na kutekeleza kanuni na wajibu wetu kama viongozi," alisema Manara.

Ofisa habari huyo aliwashukuru baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba ambao tayari walikuwa wamejitolea kuchangishana fedha kwa ajili ya kumlipia faini hiyo.

"Mimi binafsi na klabu ya Simba inawashukuru sana kwa kufanya jambo hilo, lakini nawaomba sitisheni kwa sababu klabu imeshanililipia, nawaomba tu niseme jambo hili limepita, tusonge mbele," Manara alisema.

Manara, alikuwa na hatia kwa kuingilia majukumu ya Kamati ya Katiba, Sheria na Hadhi za Wachezaji wakati wa kesi ya mchezaji Morrison kwa maneno aliyosema kupitia chombo kimoja cha habari.

Michezo
Ijumaa Septemba 18, 2020
Nipashe



Bale arejea rasmi Tottenham UKURASA 22

# SIMBA SC YAPANIA KUIPOTEZA BIASHARA

## ●●● Manara, Bocco wafunguka mchezo huo unavyotarajiwa kurejesha furaha...

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Simba ya jijini Dar es Salaam umesema umejipanga kusaka ushindi wa kishindo katika mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Biashara United kutoka Musoma itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**Akizungumza jijini jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema klabu yake imejiimarisha na kujiweka imara kuelekea mchezo huo ambao utakuwa wa kwanza kucheza nyumbani katika msimu huu mpya wa mwaka 2020/21.**

Manara (pichani) alisema wamejiandaa si tu kuvuna pointi tatu, lakini kupata mabao mengi yatakayowafurahisha wanachama na mashabiki wa klabu hiyo inayoshikilia pia taji la Kombe la FA hapa nchini.



"Nimezungumza na viongozi wetu katika benchi la ufundi ambao wameniahidi si ushindi mnono, lakini burudani safi, wamesema vijana wako tayari na kila mmoja anafurahia kurejea kwenye Uwanja wa Mkapa ambao kwetu ni nyumbani," alisema Manara.

Alisema wanaishukuru Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi kwa kuyafanyia kazi maombi yao ya kushusha viingilio katika mechi za ligi hiyo ambazo zitachezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kiongozi huyo alitaja kiingilio cha chini katika mchezo huo sasa kitakuwa ni Sh. 3,000, hivyo amewaomba mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi kuwashangilia wachezaji wao na hatimaye kuondoka uwanjani wakiwa na furaha.

"Tumepokea taarifa hizi kwa furaha kubwa, tuje kulipa hisani kwa TFF na Bodi ya Ligi, tuhakikishe tunalipa viingilio rafiki, matarajio yetu tuje kushangilia chama letu, ndio tunaanza kuwakera, tumerudi kwenye dimba kuu la Mkapa, tukitarajia mchezo mzuri, wenye idadi sahihi ya magoli, tunataka tuujaze uwanja, tuwe wengi," alisema Manara.

Naye nahodha wa Simba, John Bocco, amesema anaamini timu yao itapata mafanikio zaidi ya ilivyokuwa msimu uliopita kutokana na kikosi chao kuimarika zaidi.

Bocco alisema kila mchezaji wa Simba ana ndoto ya kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa na wanafahamu hakuna mechi rahisi.

"Naona msimu mwingine wenye mafanikio, tuko tayari kupambana ili kufikia ndoto zetu, tuko imara kwa kukabiliana na ushindani wowote," Bocco, mshambuliaji wa zamani wa Azam FC alisisitiza.

Wakati huo huo, Kaimu Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki, Hamisi Kisiwa, amewataka wadau wanaotaka kadi ya mashabiki ambao baadaye watakuwa wanahisa ni kwenda kwenye matawi yaliyo karibu na hatimaye wataandikishwa rasmi katika mfumo wa klabu.

"Ili uingie katika mfumo wa hisa, ni lazima uanzie kwenye mashabiki, lakini huwezi kufika kwenye hisa kama hukuanzia kwenye ushabiki," Kisiwa alisema.

Simba yenye pointi nne kibindoni, ilianza msimu mpya ugenini kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC jijini, Mbeya halafu ikatoka sare ya bao 1-1 na Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani, Morogoro.



Wachezaji wa Yanga kutoka kushoto ni Adeyum Ahmed, Tuisila Kisinda na Waziri Junior wakiwa pamoja baada ya kuwasili Bukoba jana, tayari kwa mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Kaitaba. **PICHA: MTANDAO**

# Mastraika Yanga waandaliwa 'dozi'

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Zlatko Krmpotic, amesema sasa amewaandalia programu mpya washambuliaji wake kutokana na kutoridhishwa na idadi ya mabao wanapata katika mechi mbili zilizopita za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Safu ya ushambuliaji wa Yanga inaongozwa na Michael Sarpong, Sogne Yocouba, Ditram Nchimbi, Deus Kaseke, Tuisila Kisinda, Haruna Niyonzima, Carlos Carlinhos na Farid Mussa.

Zlatko alisema timu yake imeanza kucheza vizuri na inamiliki mpira, lakini bado haijakaa vema kwenye idara ya kupachika mabao licha ya kutengeneza nafasi nyingi za kufunga.

Kocha huyo alisema mabao mawili ambayo wamefunga katika mechi mbili walizocheza hayatoshi na yanaifanya safu yake ya ushambuliaji kutokuwa na makali.

"Tumefunga mabao mawili tu, sijaridhika na hali hii, inaonyesha dhahiri wachezaji wangu hasa wanaocheza kwenye robo ya mwisho ya uwanja wanakosa ubunifu wa kutengeneza nafasi, nahitaji wabadilike zaidi," alisema Zlatko.

Aliongeza katika mechi dhidi ya Mbeya City walifanya mashambulizi mfululizo katika dakika 75, lakini hawakutengeneza nafasi za wazi za kufunga kama inavyotakiwa, hivyo wanahitaji kupewa mbinu zaidi za umaliziaji.

"Nimeona mabadiliko kidogo ila nalazimika tulifanyie kazi haraka kabla hatujaanza michezo yetu ya ugenini, ikiwamo mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar, tumejipanga kwenda kupambana kutafuta alama muhimu pamoja na kupata idadi nzuri ya mabao zaidi ya tulivyofanya kwenye mechi mbili zilizopita," alisema Zlatko.

Aliutaja mchezo wa kirafiki waliocheza juzi usiku dhidi ya Mlandege ya Zanzibar umemsaidia kuona wachezaji wanavyopokea mafunzo mapya na namna kila mmoja alivyotekeleza majukumu yake na hatimaye kupata ushindi wa mabao 2-0, shukrani kwa Waziri Junior na Michael Sarpong, waliofunga magoli.

Kikosi cha Yanga tayari kimeshawasili Bukoba tayari kuendelea kujinoa kuelekea mchezo wao dhidi ya Kagera Sugar, utakaochezwa kesho mjini humo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >